SUPA JACKPOT
TZS. 1,087,305,640
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 17

## DAKTARI bingwa asema wapenda ngono wanakufa mapema zaidi



Nipashe
TESA
Jumanne Machi 7, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 14
VITA VYA RUSSIA Vs UKRAINE Ushindi wake uliko, ni zaidi ya teknolojia, silaha kali za kisasa

Ukurasa 12
Acheni kutumia simu kuonyesha familia zikila chakula sebuleni

Ukurasa 13
Fahamu sababu mwanao kumaliza shule pasipo kujua chochote, hata 'a'

ELIMU
NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA
SKENDO KWA FAMILIA
Ni pale baba alipogeuka mume kwa mama na binti
•Mlezi huyo adaiwa kumpa mimba mwana anayemlea
•Aachishwa shule jicho labaki polisi, mahakama

WAKATI kinamama wanajiandaa kushangilia na kuifurahia Siku ya Wanawake Duniani, zipo familia zina machungu kutokana na mama pamoja na mabinti zake kudhalilishwa kingono na wenza wa ndoa.

Kunyanyaswa huko kunafanywa na baba mlezi au wa kambo, ambaye licha ya kufahamishwa kuwa ni mtoto wa mkewe ambaye amekubali kumlea baada ya kufunga ndoa na mama yake, mwanaume huyu anaamua kumdhalilisha binti wa kufikia.

Wanawake wanakumbushwa kuwa mtoto wa kike ni mawindo ya baba wa kambo au walezi, japo ni wenza wa ndoa wanaoishi nao.

nguvu kuanzia wakati huo Machi 22, amekuwa akinivizia kwa kila namna na kila mwanya anaoupata kunitumia kila anapotaka na kunitishia kila nikikataa. Madai yake ni kumweleza mama kuwa najipikia chakula cha peke yangu na kula mwenyewe kwa siri," anaeleza.

Anasema hali hiyo ilimchosha lakini baba yake alikuwa akimvizia akifanya hivyo nyumbani wakiwa wamebaki wawili na wakati mwingine akiwapo mdogo wangu anamtuma dukani mbali ili nibake mwenyewe na kuninyanyasa ananiita akiona nimekataa ananifuata nilipo tena ananitishia na amekuwa akinifanyia unyanyasaji chumbani kwake na mama yangu," anaeleza.

Anatamani kusoma na kufanikiwa zaidi akisema: "Bado ndoto yangu ni kusoma kuendelea na masomo na hata mama yangu ameniahidi baada ya kujifungua nitarudi darasani."

Jumanne Machi 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581242

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# MARUFUKU



Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa. Wanafunzi wakiwa bwenini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## BWENI watoto chini ya darasa la 5; muziki na video, gari la shule...

*Endelea Ukurasa wa 2*

SPECIAL SUPPLEMENT ON COMPLETION OF TWO YEARS UNDER THE ABLE LEADERSHIP OF HER EXCELLENCY DR. SAMIA SULUHU HASSAN



The Guardian Limited will publish a special supplement with **"The Guardian"** and **"Nipashe"** Newspapers, with a special report focusing on the achievements of the Government under the leadership of President **Dr. Samia Suluhu Hassan**

20th March 2023

We wish to invite you to be a part of this special supplement by publishing your **Special features, Congratulatory messages, Advertorials** and **Advertisements.**

The Guardian
Nipashe

TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON
+255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

617309101



## Lema awasilisha ombi maalum kwa Samia waliobambikwa kesi

**CHADEMA** kulamba ruzuku Bil. 3/-...

*Endelea Uk.3 & 4*

## Mlo chanzo tatizo unene, ukondefu Dar es Salaam

UKURASA 19

**MICHEZO** FEI TOTO, YANGA SC KUKAA MEZA MOJA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Serikali yapiga marufuku watoto wadogo kukaa bweni

Na Beatrice Shayo

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa waraka namba moja, mbili na tatu wa mwaka 2023 ukielekeza mambo ya msingi kufuatwa kwa wanafunzi wadogo kukaa bweni, mabasi ya shule na ukaguzi wa vitabu.

Kwa mujibu wa waraka namba mbili wa mwaka 2023 uliotolewa kwa vyombo vya habari, ukitiwa saini na Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, shule zote zinazotoa huduma ya bweni kwa madarasa ya awali hadi darasa la nne zinapaswa kusitisha huduma hiyo ifikapo Juni mwaka huu muhula wa kwanza utakapofika ukomo.

Anasema waraka huo unazuia kutoa huduma za bweni kwa wanafunzi wa elimu ya awali na darasa la nne isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa na Kamishna wa Elimu baada ya kupokea maombi rasmi kutoka kwa mdau husika.

"Maendeleo ya kweli katika nchi yoyote ile kwa kiasi kikubwa hutegemea ubora wa elimu inayotolewa katika nchi husika. Ingawa dhana ya ubora wa elimu hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine.

"Katika muktadha wa nchi yetu, elimu bora ni ile inayomjengea mhitimu uwezo wa kuchambua masuala mbalimbali kwa ufasaha ili kufanya uamuzi wenye tija, kuwa na maadili yanayoakisi mila, desturi na utamaduni, kujenga moyo wa kupenda, kuthamini na kufanya kazi ili kuleta maendeleo ya mtu binafsi, jamii na taifa kwa ujumla," anafafanua.

Mtahabwa anasema maeneo hayo matatu ni muhimu yazingatiwe katika mchakato wa utoaji elimu, ili wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu watoe mchango stahiki kwenye harakati za maendeleo ya nchi.

Anafafanua kuwa taarifa mbalimbali zilizopo kutoka kwa wadhibiti ubora wa shule na ufuatiliaji unaofanywa na wizara, unaonyesha shule nyingi zimetoa kipaumbele katika kuwafanya wanafunzi kupata ufaulu mzuri kwenye mitihani yao ya mwisho.

"Matokeo yake, kuna juhudi hafifu za kujenga maadili ya wanafunzi na kuwajengea moyo wa kupenda, kuthamini na kufanya kazi. Hali hiyo inaondoa dhana muhimu isemayo kwamba 'elimu ni maisha na maisha ni kazi'," anasema.

Alifafanua kuwa moja ya mikakati inayofanywa na shule hizo ni kuongeza ufaulu kupitia uanzishwaji wa huduma za bweni, hasa kwa madarasa ya mitihani na madarasa mengine kwa ujumla.

Anaongeza kuwa azma ya kuongeza ufaulu imedhihirika kwa shule hizo kuanzisha kambi za kitaaluma ambazo hufanyika wakati wa likizo.

Hata hivyo, anasema kuwa kambi nyingi zimebainika kuwa na mazingira hatarishi kimaadili, usalama na afya za wanafunzi kutokana na kuanzishwa bila kufuata taratibu rasmi na uanzishwaji wa bweni au makazi ya pamoja ya wanafunzi.

Mtahabwa anasema malezi na makuzi ya mtoto yanategemea mchango mkubwa unaotolewa na familia kupitia wazazi au walezi wa watoto hao.

Pia anasema imebainika kuna baadhi ya shule zimekuwa zinapokea watoto wenye umri mdogo kuanzia darasa la awali hadi darasa la nne.

"Huduma za bweni kwa wanafunzi wenye umri mdogo ikiwamo wale wa elimu ya awali na darasa la kwanza hadi la nne huwanyima watoto fursa ya kushikamana na familia na jamii zao, kujenga maadili na kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya familia na jamii zao," anasema.

Kamishna huyo anasema kulingana na utafiti uliopo, madhara ya muda mrefu yatokanayo na tabia ya kulaza watoto bweni katika umri mdogo ni watoto kukosa mapenzi kwa wazazi au walezi na jamii zao na hivyo kushindwa kuwa sehemu ya familia na jamii husika.

Anasema wizara inawakumbusha na kuwaagiza wamiliki wote wa shule kuwa huduma za bweni zitatolewa kuanzia darasa la tano na kuendelea.

Anasema hatua hiyo ni utekelezaji wa mwongozo wa uanzishaji na usajili wa shule uliotolewa na wizara Novemba mwaka 2020. Shule zote ambazo zinatoa huduma ya bweni kwa madarasa yasiyoruhusiwa zinaagizwa kusitisha huduma hiyo ifikapo mwisho wa muhula kwa kwanza mwaka 2023.

"Hairuhusiwi kwa shule yoyote ile kuwa na kambi ya kitaaluma. Hatua hii inaakisi utekelezaji wa Waraka wa Elimu Na. 3 tatu wa mwaka 2007 kuhusu kukataza kambi za masomo katika shule za msingi," anasema.

Anasisitiza kuwa ili kuhakikisha waraka huo unatekelezwa ipasavyo, kutakuwa na ufuatiliaji wa mara kwa mara kupitia wadhibiti ubora wa shule na viongozi mbalimbali wa elimu.

## USAFIRI

Kamishna wa Elimu, kupitia waraka wa kwanza, amewataka wamiliki wote wa shule zenye kutoa huduma za usafiri kwa wanafunzi, kuwa na mhudumu wa kike na wa kiume katika kila basi linalosafirisha wanafunzi kuanzia mwanzo wa safari hadi mwisho wa safari.

"Inaposhindikana, mmiliki awasilishe taarifa kupitia wadhibiti ubora wa shule kueleza sababu zilizomfanya ashindwe kufanya hivyo," anaelekeza.

Mtahabwa pia alielekeza wamiliki wa shule waache kuweka muziki, nyimbo na picha za video zinazokwenda kinyume cha maadili, mila, desturi na utamaduni, badala yake waweke muziki au nyimbo na picha za video zinazojenga maadili na uzalendo kwa wanafunzi.

"Ili kukomesha vitendo vya ukatili kwa wanafunzi wakiwa kwenye magari na mabasi, kunapaswa kuwa na ratiba rafiki za safari ili wanafunzi, hususani watoto wadogo, wapate muda wa kutosha kupumzika kwa ajili ya



ukuaji wao," anaelekeza.

Pia anaelekeza magari au mabasi yawe na vioo angavu na waajiriwa wawe wenye uadilifu.

## VITABU NA VIFAA

Kupitia waraka wa elimu namba tatu, Kamishna wa Elimu ametaka walimu na wakufunzi wa taalum kwenye shule na vyuo vya ualimu mtawalia, kuweka utaratibu wa kukagua vitabu na vifaa mbalimbali vya kujifunza na kufundisha walivyonavyo wanafunzi, ili kudhibiti uingizwaji na matumizi ya vitabu na vifaa vinavyokwenda kinyume cha maadili, mila, desturi na utamaduni.

Alisema shule au chuo cha ualimu kikipokea msaada wa vitabu au vifaa vyovyote vya kujifunza, itatakiwa kushirikisha wadhibiti ubora wa shule kwenye eneo husika, ili kufanya ukaguzi wa vitabu au vifaa hivyo kabla ya kuanza kutumika shuleni au chuoni.

Mtahabwa alisema Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA) iweke utaratibu wa kukagua vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia inavyopokea kama msaada ili kuhakikisha vina maudhui stahiki.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Elimu, utekelezaji wa waraka huo ulianza Machi Mosi mwaka huu.

## MAONI YA WADAU

Mmoja wa wazazi, Mussa said, alisema anaunga mkono waraka wa kwanza kwa kuwa kumtenganisha mtoto na wazazi wake kuanzia chekechea kunamnyima muunganiko na wazazi, mila, desturi na malezi.

Pia alisema inamnyima kuwa na uchungu na wazazi wake kwa kuwa muda mwingi anaishi na watu ambao sio wazazi wake na ni rahisi kuchukua tabia za anayemlea. Alisema kuwa mara nyingi umri wa watoto kuanzia chekechea hadi darasa la nne ni wa kujifunza mambo mbalimbali kutoka kwa wazazi, ambayo yanasaidia kujenga uhusiano kati ya familia na mtoto.

"Tunaipongeza serikali kwa uamuzi huu, pamoja na kwamba tumechelewa lakini ni heri tuchelewe lakini tutimize malengo yatakayosaidia jamii kuchukua wajibu wa malezi unaofaa," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
06.03.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 09-03-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Chalinze,** gari hizo zina namba za usajili: **T 308 EAG / ZD 9920**
**T 133 CCP / T 922 DZA T 204 DYJ / T 161 BDU**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu** - **mita 42**
**Upana** - **mita 4.70**
**Kimo** - **mita 5.50**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Chalinze kupitia Bagamoyo,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217312502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe: 06/03/2023

**TAARIFA KWA UMMA**

11. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumanne tarehe 07-03-2023** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **DODOMA**, Gari hilo lenye namba za usajili:
**T 175 DFN/T 168 DFN**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu** - **mita** **18:00**
**Upana** - **mita** **2.80**
**Kimo** - **mita** **5.00**

3. Njia itakayotumika **DAR ES SALAAM hadi DODOMA kupitia MOROGORO.** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***( kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217312102

**HABARI KITAIFA**

# Lema awasilisha ombi kwa Samia waliobambikwa kesi

**Christina Mwakangale na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kumfutia kesi na kumwezesha kurudi nchini.

Aidha, amemwomba kuangazia zaidi mfumo wa utoaji haki ambao unafanya watu wasio maarufu kukosa haki na kwamba sulushisho ni Katiba mpya.

Lema aliyasema hayo jana wilayani Karatu, Mkoa wa Arusha, akiendelea na ziara yake maeneo tofauti pamoja na kuzungumza na wananchi, tangu arejee nchini wiki iliyopita akitokea uhamishoni nchini Canada.

Alisema Rais Samia amemfurahisha baada ya kutoa kauli kwamba wapinzani sio maadui,

"Kweli nilimwambia mama (Rais Samia) nataka kuja Tanzania, ila walinifungulia kesi mimi utafikiri mimi mwenyewe ndio mahakama, zikafutwa. Nataka nitumie fursa hii kumshukuru, lakini jambo moja mheshimiwa rais afikirie, mimi ni kiongozi wa kisiasa, viongozi wangu, mimi mwenyewe nimepata fursa, kupigania haki yangu, hata kupitia kwake," alisema Lema.

Alisema kwamba, kutokana na nafasi yake ya uongozi kisiasa ikiwamo vongozi wengine kwenye chama chake, ilikuwa rahisi kumfikia rais, akisema kwa wasio na fursa hiyo ni wengi ambao alidai hubambikiwa kesi na kushindwa kupata haki zao.

"Watu maskini ni wengi ambao wapo Magereza wamebambikiwa kesi, hawawezi kuwa na access (upatikanaji) ya kukufikia wewe, wala wazazi wao hawa wanahitaji Katiba mpya," aliongeza Lema.

Alisema uwapo wa katiba hiyo utasaidia kuwa na sheria zinazotoa ulinzi kwa kila Mtanzania na haitakuwa kigezo cha mtu yeyote kuamua kumbambikia kesi pasi na ushahidi.

"Sheria bora inahitajika, mimi nilikuwa nimeonewa na kesi zikafutwa ni kwa sababu ya maridhiano, ili pasitokee mtu wa kuonewa tunahitaji Katiba mpya."

"Hapa (Karatu) hakuna mtu mwenye jina kama Lema, hawa unaweza usiwajue, mheshimiwa Rais ili uwasaidie wanahitaji Katiba, polisi iwe na nidhamu na ofisi ya mashtaka iache kubambikia watu kesi," alisema Lema.

**BODABODA**

Kuhusu usafiri wa bodaboda, alisema imetafsirika kama sura iliyobeba umaskini akisema sio kazi ambayo inapaswa kuungwa mkono na vijana, kwa kuwa athari zake ni kubwa.

"Hii sio kazi, ajira ya kuunga mkono vijana, kwani ina ujira duni na imeua vijana wengi na athari zake katika afya ni mbaya. Kazi hii haipaswi kuwa usafiri wa umma, nchi inaweza kujiondoa kutoka katika umaskini huu kama tukijali vyema," alisema Lema.

Alisema kutokana na suala la bodaboda kuchukua sura na taswira tofauti, ataendelea kuelimisha wananchi pamoja na suala la VICOBA.

**LISSU**

Akizungumza kupitia mtandao wa 'Club House', Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Tundu Lissu, aliungana na Lema akisema biashara ya bodaboda inatokana na ukosefu wa ajira.

"Nikitumia lugha ya upole naweza kusema kwamba hili linafanyika kwa namna ya kuficha tatizo la ukosefu wa ajira nchini. Ni namna ambayo vijana wamelazimishwa kuishi kwa sababu serikali imeshindwa kutatua tatizo la msingi la ajira," alifafanua Lissu.

## Mpango ataja njia kukabiliana umaskini nchi zinazoendelea

**Na Jenifer Gilla,** DOHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, ametaja njia mbili zitakazosaidia nchi maskini (LDC) kuharakisha utekelezaji wa Mpangokazi wa Doha (DPoA) wenye lengo la kuzisaidia nchi hizo kukabiliana na umaskini na kufikia malengo endelevu.

Alitaja malengo hayo kuwa ni mageuzi ya kisera, kitaasisi na udhibiti yanayolenga kukuza uchumi na kuchochea maendeleo ya sekta binafsi, viwanda, elimu, afya na miundombinu hasa umeme, reli, bandari na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Vilevile, mageuzi hayo yavutie uwekezaji wa teknolojia ya kijani ikiwamo sekta ya kilimo hasa inazoongozwa na vijana na wanawake, ili kuongeza fursa ya ajira katika kundi hilo na kuchangia kuleta maendeleo ya nchi.

Alitaja mbinu ya pili ni kuanzisha ubia wa kimkakati wa kikanda, kiserikali na kimataifa na kuongeza ufadhili wa kiuchumi wa masharti nafuu pamoja na mambo mengine mbinu hizo zimeisaidia Tanzania kupiga hatua za kimaendeleo na sasa inakaribia kuhitimu katika kundi la nchi zenye kipato cha chini.

Mpango aliyasema hayo juzi alipohutubia viongozi wa nchi hizo katika Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinaoendelea za Kipato cha Chini (UNLDC5) unaondelea Doha nchini Qatar na kuongeza kuwa njia hizo pia zimeisaidia kuwa na mwelekeo mzuri wa kiuchumi kwa kipindi cha miaka 10 licha ya kupitia changamoto mbalimbali ikiwamo athari za mabadiliko ya tabianchi na UVIKO -19.

"Tanzania imepiga hatua kubwa tangu mkutano wa nne wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea za Kipato cha Chini (LDC4), uchumi wetu unasalia kuwa thabiti wenye mwelekeo mzuri. Ni moja ya nchi zinazokua kwa kasi kiuchumi katika ya nchi za Jangwa la Sahara zilipo katika kundi la nchi zenye kipato cha chini," alisema Mpango.

Alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kuwa ni farihisi ya maendeleo ya binadamu imeongezeka kutoka 0.41 mwaka 2002 hadi 0.55 mwaka 2021, umri wa kuishi uliongezeka kutoka miaka 60 mwaka 2010 hadi miaka 67.2 mwaka 2022, idadi ya watoto chini ya miaka mitano ambao wana utapiamlo (waliodumaa) ilipungua kutoka asilimia 42 mwaka 2010 hadi asilimia 30 mwaka 2022.

Aidha, alisema kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka mitano kilipungua kutoka vifo 81 mwaka 2010 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2022, kiwango cha vifo vya uzazi kilipungua kutoka vifo 432 mwaka 2015 hadi 250 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2021 na maambukizi ya malaria kwa watoto wenye umri wa miezi sita hadi 56 yalipungua kutoka asilimia 18 mwaka 2007/08 hadi asilimia nane mwaka 2021/22.

Alisema pia wameboresha ubunifu wa kifedha kidijitali na sasa unafanyika kwa simu za mkononi, kuondoa ada katika elimu ya msingi na sekondari, kuongeza kiwango cha uandikishaji shule za msingi kutoka asilimia asilimia 85 mwaka 2015 hadi asilimia 97 mwaka 2021.

Akizungumza katika mkutano huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres, alisema nchi hizo zinahitaji msaada wa haraka ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, ikiwamo kutokomeza umaskini, uhakika wa chakula na upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira.

Kwa siku sita Tanzania pamoja na nchi nyingine 45 zipo nchini Qatar zikijadili utekelezaji wa DPoA ambao umewekea mkazo mambo muhimu matano, ikiwamo elimu ya chuo kikuu kutolewa kwa njia ya mtandao ili kukuza ubora wa elimu, kujengewa uwezo kuboresha usalama wa chakula, ushirikiano na nchi zinazoendelea katika kuleta maendeleo.

Mengine ni kuwapo na kituo cha msaada wa kuongeza uwezo wa kustahimili athari za mabadiliko ya hali ya hewa kupitia urekebishaji na uboreshaji wa mfumo wa tahadhari kama vile kujengwa madaraja, kuta za kuzuia maji ya bahari kuvamia makazi na kuboresha miundombinu ya barabara.

Mpango huo utasaidia nchi hizo kukabiliana na vikwazo vinavyorudisha nyuma juhudi za kupiga hatua za maendeleo ikiwamo kukosekana kwa utoaji wa elimu bora, kukosa usaidizi wa kuhitimu katika kundi la nchi zenye kipato cha chini, kukabiliana na usalama wa chakula na mfumuko wa bei za vyakula na msaada katika uwekezaji.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
THE CITY COUNCIL OF DODOMA
CCD

## TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala Iugala, Nala Segu kukamilisha malipo ya viwanja hivyo mapema.

Mwananchi au taasisi itakayoshindwa kulipia kiwanja hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2023 atambue kuwa kiwanja hicho kitauzwa kwa mteja mwingine ili kuboresha huduma katika Halmashauri bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**

Joseph C. Mafuru
**MKURUGENZI WA JIJI**
**DODOMA**

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S. L. P. 1249,
DODOMA

217303602

# Lissu afunguka CHADEMA kupokea ruzuku Bil. 3/-

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema chama hicho kimekubali kupokea ruzuku ya Sh. milioni 102 kwa mwezi.

Ikiwa chama hicho kitapokea kiasi hicho cha fedha, kitapata zaidi ya Sh. bilioni 2.9 ambayo ni ruzuku kwa kipindi cha kuanzia Novemba 2020 hadi Machi mwaka huu.

Lissu alitoa kauli hiyo wakati akiulizwa maswali na wananchi mbalimbali kwenye mtando wa Club House jana na kufafanua kuwa fedha hizo wameanza kuzipata mwezi huu na wameahidiwa kulipwa malimbikizo yote ya nyuma.

"Tulijulishwa katika kikao cha Kamati Kuu kwamba ruzuku imeanza kulipwa kwa mara ya kwanza mwezi huu kwa kulipa malimbikizo ya nyuma, haijalipwa yote lakini imeanza kulipwa.

"Hili la ruzuku litaelezwa vizuri na Katibu Mkuu wa chama wakati wowote," alisema Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria.

Lissu pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoendesha maridhiano, akisisitiza kuwa haijawahi kutokea.

Juzi, Nipashe ilimuuliza Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe kuhusu ruzuku, akielekeza suala hilo litolewe ufafanuzi na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema, naye akisema litajibiwa na John Mnyika, Katibu Mkuu wa CHADEMA.

Jana alitafutwa tena na kusisitiza kuwa Mnyika atalizungumzia suala hilo. Nipashe ilipomtafuta Katibu Mkuu, Mnyika, alisema: "Nitawaita waandishi wa habari (hakutaja siku) kulizungumzia hilo. Kwa sasa siwezi kusema lolote".

Alipoulizwa kuhusu kauli ya Lissu kueleza kuwa wameshapokea fedha hizo, Mnyika alisema "andikeni alichosema Lissu, mimi nitazungumza wakati ukifika."

Katika ufafanuzi wake, Lissu alisema kuwa baada ya uchaguzi mkuu mwaka 2020, chama hicho kimeishi katika mazingira magumu, ikiwamo baadhi ya maofisa walikuwa wameajiriwa kwenye ofisi za chama hicho kuanza kukimbia na kukimbilia chama kingine cha siasa.

Pia alisema kutokana na kutokuchukua ruzuku, ili kujiendesha, chama hicho kimekuwa kinajiendesha kwa michango ya wanachama na wahisani wengine.

"Na ndiyo maana shughuli zetu nyingi tumekuwa tukiziendesha tofauti na miaka mingine kutokana na hali ya uchumi," alisema.

Lissu ambaye amewahi kuwa Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), alisema sababu za chama hicho kupokea ruzuku zitaelezwa zaidi katika taarifa itakayotolewa na Katibu Mkuu wa chama hicho japo aliweka bayana kwamba miongoni mwa kilichowasukuma ni kutokana na dalili njema ya mazungumzo ya maridhiano yanayoendelea kati yao na serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Tumepokea kwa sababu kuna uwezekano kwa hayo ambayo yamefanyika kwa mwaka mzima ya kuwa na utaratibu utakaotuondoa kwenye namna hii ya kuendesha nchi na uchaguzi tuliyokuwa tunalalamikia, sio kwamba tumekubaliana na uchaguzi mkuu uliopita.

"Tunapata ruzuku kutokana na asilimia 50 ya mbunge wa jimbo na asilimia 50 inayotokana na asilimia 17 ya kura za wabunge.

"Katika kipindi chote hiki ambacho hatukuwa na ruzuku, Katibu Mkuu na wengine waliobaki kwenye chama wameishi katika mazingira magumu sana na wengine walivyoona mshahara umeisha, waliondoka.

"Katika kipindi chote ambacho hatukupokea ruzuku, chama kilijiendesha kwa sababu wanachama wamejitolea.

"Tumekuwa na mazungumzo na nimepata kuhudhuria kikao kimoja cha maridhiano, tunazungumza, sasa hivi yale masuala ya msingi ambayo tulisema haya yanatakiwa yashughulikiwe, ili turudi katika hali ya kawaida ya kisiasa, yapo yaliyoshughulikiwa na ambayo bado lakini yanazungumzwa.

"Kwa hiyo, ni sahihi kusema kwamba mazingira ya kisiasa ya sasa ni tofauti na yalivyokuwa miaka mingine wakati Rais Samia anachukua madaraka, tumeingia katika hatua mpya katika siasa zetu ambayo inaonyesha japokuwa bado kuna kazi kubwa inayotakiwa kufanyika, lakini angalau kuna huo mwanzo wa kuanza 'kudili' nayo ambayo yalikuwa ni magumu katika nchi yetu.

"Tumepita kurasa mbaya kabisa katika historia ya nchi yetu, lakini hatua za mwanzo zinaonyesha dalili njema tumechukua ruzuku kwa sababu ya dalili njema na zipo nyingine zinakuja," alifafanua.

Kuhusu kushiriki uchaguzi mkuu ujao, Lissu ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Singida Mashariki, alisema msimamo waliokuwa nao awali wa kutokushiriki maridhiano, wameuondoa kutokana na namna wanavyoona maridhiano yanavyoendelea.



Mwenyekiti wa Wanawake Tughe, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Susan Reuben (kushoto), akimfariji mtoto Abdulrasul Jumanne (12), anayesubiri kufanyiwa upasuaji wa moyo kwenye Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. WCF imetoa misada ya mahitaji mbalimbali na fedha za kugharimia upasuaji wa moyo kwa watoto watatu wenye uhitaji wanaopatiwa matibabu kwenye taasisi hiyo. Msaada huo ni sehemu ya sherehe za Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dereva wa lori kizimbani mashtaka kusababisha vifo

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

DEREVA wa lori la makaa ya mawe lenye namba za usajili T 305 EAR na Tera lenye namba za usajili T918 EAZ, mali ya Kampuni ya Spesho Raizd, Karim Gulam (38) amefikishwa mahakamani akituhumiwa kusababisha vifo vya watu watatu.

Mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya, Mwendesha Mashtaka, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Stephen Msongaleli alidai kuwa katika kesi hiyo, mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo Februari 17, mwaka huu kwenye Kijiji cha Msagula wilayani hapa.

Alidai kuwa kwa makusudi aliendesha chombo cha moto kwa mwendo wa hatari kwenye barabara ya umma na kusababisha vifo.

Alidai kuwa kwa kufanya hivyo, alifanya kosa kinyume cha kifungu Na. 40(1)(a) na 27(1) vinaelekeza kunyang'anywa leseni kwa kipindi cha miaka mitatu endapo atapatikana na hatia ya kosa hilo na namba 63(2)(a) cha Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 na marejeo ya mwaka 2002.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mshtakiwa alikana kufanya kosa hilo. Kesi hiyo itatajwa tena mahakamani huko Machi 24, mwaka huu.

Inadaiwa kuwa dereva huyo aligonga pikipiki iliyokuwa imebeba watu watano na kusababisha vifo vya Rashid Issa (15), Bashira Issa (15) na Magesa Charles (15), wote wanafunzi wa kidato cha pili na kuwajeruhi Ozra Abduli na Craudi Abdul (1) ambao walikuwa wakisafiri kwa kutumia pikipiki hiyo.

# Ajali yaua watatu, wamo polisi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WATU watatu, wakiwamo askari polisi wawili, wamefariki dunia katika ajali iliyotokea Kata ya Mboga, Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani.

Kamanda wa Polisi mkoani Pwani, Pius Lutumo, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo iliyotokea juzi majira ya saa 11:45 alfajiri huko maeneo ya Mavi ya Ng'ombe, Kijiji cha Mboga, Kata ya Msoga, Tarafa ya Chalinze, Wilaya ya Kipolisi Chalinze.

Akielezea tukio hilo juzi, Kamanda Lutumo alisema gari lenye namba za usajili T 323 BAL aina ya Toyota Crestar, likiendeshwa na Mkaguzi Msaidizi wa Polisi wa Kituo cha Chalinze, Ndwanga Dastani (28), akitokea Chalinze kuelekea Lugoba, liliacha njia kutoka upande wa kushoto wa barabara na kwenda upande wa kulia na kugonga karavati kisha gari hilo kupinduka na kusababisha vifo vya watu watatu.

Aliwataja waliofariki katika ajali hiyo kuwa ni Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Dastani, Askari Polisi wa Kituo cha Polisi Chalinze, Konstebo Emmiliana Charlse (26) na Karimu Simba (27) aliyekuwa karani wa Mahakama ya Wilaya ya Lugoba.

Kamanda Lutumo alisema majeruhi wa ajali hiyo ambaye ni Askari wa Polisi Kituo cha Chalinze, Konstebo Mwanaidi Shabani (25) amebainika kuumia maeneo mbalimbali ya mwili wake na amepelekwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kwa matibabu zaidi.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi na dereva kushindwa kulimudu gari na kupinduka na kusababisha vifo hivyo, majeruhi mmoja na uharibifu wa gari hilo.

# ‘Waandishi wa habari toeni maoni muswada kufumua Sheria Habari’

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC), Samson Kamalamo, amehimiza waandishi wa habari kutoa maoni kuhusu muswada unaolenga kufanya mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari, 2016.

Kamalamo alitoa rai hiyo jana jijini alipozungumza na mwandishi wa habari kufuatia serikali kuwasilisha bungeni hivi karibuni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo.

“Kwa kuwa muswada wa sheria hiyo unatarajia kuwa sheria itakayosimamia waandishi wa habari nchini, njia pekee ya kupata sheria bora ni waandishi wa habari kutoa maoni yao kila watakapopata fursa ya kufanya hivyo ili mwishowe nchi iwe na sheria bora.

“Pamoja na hayo, ninaomba ieleweke kwamba, sekta ya habari kwa sasa iko katika harakati za kutaka kutambuliwa kama sekta rasmi likiwamo suala la waandishi wa habari kulipwa mishahara wanayostahili kwa mujibu wa elimu zao na uzoefu wao kazini.

“Wakati hayo yakiendelea, lazime tuelewe kwamba, ili tuwe na sheria nzuri katika nchi yetu, lazima sisi waandishi wa habari tujitokeze kwa wingi kadri tutakavyoweza kutoa maoni kwa watakaokuwa wakikusanya maoni ya muswada huo.

“Ninayasema haya kwa sababu hata Waziri Nape (Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari), ameshatushauri sisi waandishi wa habari tutoe maoni ya muswada huo ili mwishowe tupate sheria nzuri.

“Hivyo basi, waandishi wa habari tusikae kimya, tutimize wajibu wetu kwa kutoa maoni badala ya kukaa kimya na kusubiri watu wengine waje watusemee.

“Kama tutalitimiza hilo, kisha serikali ikapuuza maoni yetu, basi itakuwa rahisi kwetu kuendelea kupiga kelele hadi hapo maoni yetu yatakapozingatiwa,” alisema Kamalamo.

Wadau wa habari nchini wamekuwa wakiilalamikia Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 kwa kipindi kirefu kwa kile kinachoelezwa kwamba ina vifungu vinavyokandamiza uhuru wa habari.

Wakati wa Mkutano wa 10 wa Bunge, serikali iliwasilisha bungeni jijini Dodoma muswada unaolenga kufanya mabadiliko ya sheria hiyo.

# Chongolo kumshtaki waziri

**Na Augusta Njoji,** MBULU

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ametishia kumshtaki kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kutokana na kutoshughulika ipasavyo kwenye ujenzi wa barabara ya Mbulu-Haydom hadi Singida yenye urefu wa kilometa 25 kwa kiwango cha lami.

Pia ameonyesha kukerwa na ubovu wa barabara ya Orbesh hadi Haydom wilayani Mbulu na kumwagiza Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kupeleka fedha za dharura za kuitengeneza ili kuwaondolea adha wananchi.

Chongolo alitoa kauli hiyo jana kwenye ziara yake aliyoambatana na sekretarieti ya chama hicho alipozungumza na wananchi wa kata za Hyderer, Labay na Haydom.

Alisema mkandarasi amepewa jukumu la kujenga barabara kwa urefu huo lakini fedha haijatoka hadi sasa.

“Kama wameweka kilometa 25 na hawajatoa fedha, wamejitengenezea nongwa, ninakwenda kuwaagiza waongeze na kilometa 25 iwe 50 na fedha zitoke haraka, hatuwezi kuwa tunawaambia wananchi tunaleta, tunaleta wanataka kuona vimefika.

“Niwaambie leo (jana) nimezungumza kwa kirefu na Rais Samia lakini nimeanza kuchochea kidogo kwamba huyu Waziri wa Ujenzi bado hajaanza kushughulika kikamilifu na barabara ya Mbulu-Haydom hadi Singida na yeye akaniambia nenda kaone kwa upande wa Mbulu nini kinaendelea halafu jioni tutazungumza.

“Jioni (jana) nitamaliza hadithi ya hii fedha kufika hapa, ndio kazi ya serikali. Kama mimi nina fursa ya kumfikia Rais, ni kazi ndogo tu kumwambia Rais, waziri hajafikisha fedha hata nikimchukua Kheri James anaweza kufanya, bahati mbaya sasa hivi zamu yangu ndio ninaifanya.

“Kazi hii ninaiweza na nipo timamu wala mbunge huna sababu ya kwenda kuruka sarakasi, nitatumia mdomo wangu,” aliahidi.

Alisema CCM haiko tayari kuona watu wanaopewa dhamana wanashindwa kutekeleza mipango iliyoahidiwa kwa wananchi kwa kukaa kienyeji.

“Tunataka wakae sawa, watambue wajibu wao wa kuleta matokeo yawe tija kwa wananchi,”alisema.

Kuhusu barabara ya Orbesh hadi Haydom, Chongolo alisema: “Nimekuja na hii barabara sijafurahishwa nayo, barabara ni mbovu haifanani na shughuli za maendeleo, niwaambie wasituletee hadithi ya bajeti, tunataka barabara itengenezwe iwekewe changarawe ili ipitike wakati wote”.

Chongolo pia alisema serikali kupitia ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025, imedhamiria kutokomeza vifo vya kinamama na watoto kwa asilimia 100 na ndio sababu ya kila kituo cha afya kinachojengwa majengo ya wodi za kinamama na vyumba vya upasuaji yamepewa kipaumbele.

“Nimeshapita mikoa 18 na kazi yangu ni kukagua pia kwenye vituo vya afya ili kuona mambo tuliyoyapa kipaumbele kama yamefanyika na ninasisitiza maeneo ya hospitali miti ya matunda ipandwe,” aliagiza.

Awali, Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Massay, alisema barabara hiyo ilianza kujengwa kwa Sh. bilioni 37 kwa kipande kidogo cha kilometa 25.

“Nikuombe Katibu Mkuu kwa sababu mkandarasi hajapewa fedha zozote na wewe umekuja na ndio muuza duka, tusaidie kuhakikisha ile barabara yote ijengwe kwa kiwango cha lami,” alisema.


## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Adili Auction Mart Ltd,Frostee Attorneys,Gadau Auction Mart & Majembe Auction Mart** Kwa idhini tuliyopewa na **AMANA BANK LTD** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa wadaiwa wote na wadhamini mlipe madeni yenu yote kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. Mnada utafanyika mahali ilipo dhamana.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA NA MAHALI ILIPO**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | GADIEL J MAEDA | NYUMBA | KIRANYI,SAKINA,ARUSHA | 10/04/2023 Saa07:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 2 | NEEMA C MASSAWE | NYUMBA | OLOSIVA,OLORIEN,ARUSHA | 10/04/2023 Saa04:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 3 | VUMILIA M NDAISHAU | NYUMBA | OLNJAVUTIAN,SINONI,ARUSHA | 12/04/2023 Saa07:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 4 | MAHDIA JUMA NZOMKUNDA | NYUMBA | MLIMANI,SINONI,ARUSHA | 03/04/2023 Saa08:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 5 | MOHAMMED H OTHMAN | NYUMBA | OLKEREYAN,OLASITI,ARUSHA | 12/04/2023 Saa05:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 6 | ABUBAKARI I JAMBIA | NYUMBA | LONGDONG,SOKONI I,ARUSHA | 10/04/2023 Saa04:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 7 | LAURENCE B CHAMI | NYUMBA | KAMBI YA CHUPA, BARAA,ARUSHA | 19/04/2023 Saa04:00 | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 8 | FATUMA M MJEMA | NYUMBA | OLNJAVUTIAN, SINONI,ARUSHA | 28/04/2023 Saa07:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 9 | RAYMOND G MBWAMBO | NYUMBA | MURIET, MURIET,ARUSHA | 18/04/2023 Saa04:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 10 | JUMANNE H MWAMEDI | KIWANJA | VIKINDU | 23/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 11 | AMOUR HAJI OMAR | NYUMBA | VIJIBWENI KIGAMBONI | 25/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 12 | RASHIDI I BAKARI | NYUMBA | MBAGALA RANGI TATU | 30/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 13 | MEGACJ SOLUTIONS | NYUMBA | PLOT NO 168 KBVII CHUMBAGENI, TANGA CITY | 1/04/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Frostee Attorney Mawasiliano:0673173156 |
| 14 | RAHAMI AGRICULTURE INVESTMENT LTD | NYUMBA/KIWANJA | PLOT P 24205 BOKO MAGENGENI, DAR ES SALAAM | 18/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Frostee Attorney Mawasiliano:0673173156 |
| 15 | SALMA MOHAMED UBWA | KIWANJA | PLOT NO. 2523 BLOCK A MBUTU | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Gadau Auction Mart &CO LTD Mawasiliano: 0675993420 |
| 16 | ALSAID GLASS CENTER | NYUMBA | PLOT NO. 224 BLOCK A MAJOE | 01/04/2023 SAA4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Gadau Auction Mart &CO LTD Mawasiliano: 0675993420 |
| 17 | GLITTER GEMS LTD | NYUMBA | PLOT NO. 1301 Msasani Penisula Areas | 25/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Frostee Attorney Mawasiliano:0673173156 |
| 18 | ZAKIA MOHAMED JUMA | NYUMBA | DEGE AREA KIGAMBONI | 22/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | Gadau Auction Mart &CO LTD Mawasiliano: 0675993420 |
| 19 | MARY MOSES NGWANANOGU | NYUMBA | STOPOVER, KARANGA, UBUNGO | 07/04/2023 Saa05:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 20 | RAHAMI AGRICULTURE INVESTMENT LTD | KIWANJA | PLOT NO.91 BLOCK “F” KAREGE MANOFU AREA | 18/02/2023 SAA 6:30 MCHANA NA KUENDELEA | Frostee Attorney Mawasiliano:0673173156 |

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
2) Ukaguzi wa dhamana utafanyika siku nne kabla ya mnada kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana.
3) Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4) Dhamana itauzwa “kama ilivyo”

***WOTE MNAKARIBISHWA***

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**
**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**

**ADILI AUCTION MART LTD,**

**LIMITED**
**MAKUMBUSHO**
**DAR ES SALAAMS L P 40616,**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**

**MAJEMBE AUCTION MART LTD,**
**LIMITED**
**S L P 70708,**
**DAR ES SALAAM**

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**GADAU AUCTION MART CO LTD**
**P.O.BOX 40855, DAR ES SALAAM**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**FROSTEE ATTORNEYS**
**P.O.BOX 70950, DAR ES SALAAM**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Amana Bank Ltd**
**S L P 9771**
**SIMU: +255 (022) 2129013**
**DAR ES SALAAM**

*217311902*

## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Adili Auction Mart Ltd,Nutmeg Auctioneer,Gadau Auction Mart & Majembe Auction Mart** Kwa idhini tuliyopewa na **AMANA BANK LTD** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa wadaiwa wote na wadhamini mlipe madeni yenu yote kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. **Mnada utafanyika mahali ilipo dhamana.**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA INAYOUZWA | MAHALI DHAMANA ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA | MUUZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FEDSON MYAGA MISANA | NYUMBA | KANINDO STREET / KISHIRI WARD NYAMAGANA MINICIPAL | 20/03/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 2 | TOBIAS B TOBIAS | NYUMBA | IBINZA STREET / BUSWELU WARD, ILEMELA MUNICIPAL | 23/03/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 3 | PRISCA A KAIJAGE | NYUMBA | KAGERA STREET / LWANIMA WARD, NYAMAGANA MUNICIPAL | 20/03/2023 SAA 6 MCHANA NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 4 | MSHINDO HAJI SHAHA | NYUMBA | BULOLA 'B' / BUSWELU WARD, ILEMELA MUNICIPAL | 23/03/2023 SAA 6 MCHANA NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 5 | MANYAMA M MAKANKILA | NYUMBA | PASIANSI MAGHARIBI STREET/ PASIANSI WARD ILEMELA WARD | 27/03/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 6 | ISIHAKA ABDUL CHIBWANA | NYUMBA | KISEMVULE DAR ES SALAAM | 23/03/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 7 | ISSA ABDULLAH ALLY | NYUMBA | SENJE, MSALATO AREA DODOMA | 27/03/2023 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA | Adili Auction mart Mawasiliano simu: 0717 084 658 |
| 8 | RASHID J SAID | NYUMBA | MAGOMENI MAKUTI DAR ES SALAAM | 28/03/2023 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA | Nutmeg Auctioneer and property Simu 0754497396 |
| 9 | ZEERAQ TRADERS LIMITED | NYUMBA | KANGE, TANGA | Tarehe 23/03/2023 Saa06:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 10 | RAMADHANI M KIULA | NYUMBA | MLIMANI, MURIET,ARUSHA | 23/03/2023 Saa05:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 11 | OLAICE B LUKUMAY | NYUMBA | SAMANGA, ELERAI,ARUSHA | 27/03/2023 Saa04:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 12 | MATHEW N KAAYA | NYUMBA | AKHERI, MAKINGA,MERU,ARUSHA | 28/03/2023 Saa04:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 13 | SUDI HUSSEIN KWEKA | NYUMBA | OLOSIVA,SAKINA,ARUSHA | 29/03/2023 Saa04:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 15 | YUSUFU RAMADHANI ALLY | NYUMBA | OLKEREYAN,OLASITI,ARUSHA | 27/03/2023 Saa07:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 16 | RAJAB ALLY NZOMUKUNDA | NYUMBA | OLASITI,OLASITI KATI,ARUSHA | 03/04/2023 Saa07:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 17 | FAHIM KARAMA AHMED | NYUMBA | KIRANYI,SAKINA,ARUSHA | 05/04/2023 Saa07:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 18 | HARUB S SULEIMAN | NYUMBA | OLNJAVUTIAN,SINONI,ARUSHA | 04/03/2023 Saa04:00 Asubuhi | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 19 | CHARLES L MEDIRI | NYUMBA | OLNJAVUTIAN,SINONI,ARUSHA | 03/04/2023 Saa07:00 Mchana | Majembe Auction mart Ltd/ Mawasiliano: 0754 475 932 / 0767 608 090 |
| 20 | ANGELA G MUSHI | NYUMBA | MTAA WA SALASALA,KATA YA WAZO | 05.04.2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA | Gadau Auction Mart &CO LTD Mawasiliano: 0675993420 |

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
2) Ukaguzi wa dhamana utafanyika siku nne kabla ya mnada kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana.
3) Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4) Dhamana itauzwa ***“kama ilivyo”***

***WOTE MNAKARIBISHWA***

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**

**ADILI AUCTION MART LTD,**
**LIMITED**
**MAKUMBUSHO**
**S L P 40616,**
**DAR ES SALAAM**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**

**MAJEMBE AUCTION MART LTD,**
**LIMITEDS L P 70708,**
**DAR ES SALAAM**

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD**
**P.O.BOX 14216**
**ARUSHA**
**MKURUGENZI MTENDAJI**

**GADAU AUCTION MART CO LTD**
**P.O.BOX 40855, DAR ES SALAAM**

**AU**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**Amana Bank Ltd**
**S L P 9771**
**DAR ES SALAAM**
**SIMU: +255 (022) 2129013**

*217312002*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Rais Samia kwa kuonesha uzalendo

**KATIKA** kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8 (kesho), Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), limeandaa kongamano ambalo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Rais Samia atazungumza na Watanzania kupitia kongomano hilo la kitaifa, litakalofanyika mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Hatua ya Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kukubali kuwa mgeni rasmi katika kongomano hilo lililoandaliwa na wanawake wa chama cha upinzani ni ya kizalendo ambayo inaonesha anawatumikia wananchi wake bila kujali itikadi za vyama wanavyotoka.

Utayari wa rais kuhudhuria kongamano akiwa ni kiongozi wa kwanza mwanamke kushika wadhifa huo wa juu, inaleta matumaini makubwa kwa nchi kuishi kwa maelewano na kusikilizana pande zote kwa maendeleo ya taifa.

Taarifa za Rais Samia kuhudhuria kongomano hilo zilitolewa na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha na kusema namna walivyofanyakazi na rais, wameamua kumwalika na yeye amekubali kuhudhuria kongamano hilo ili asikilize kinamama wa chama hicho na upinzani wanavyosema.

"Nimefurahi kwamba amekubali kuja kusikiliza changamoto, huo nao ni ujasiri, kwa sababu yeye ni kiongozi wa serikali ana haki ya kuwahudumia wananchi wote wa vyama vyote."

Kila mara Rais Samia anapokuwa kwenye majukwaa ya mikutano amekuwa akisisitiza umuhimu wa vyama kushirikiana na kuwa upinzani sio uadui kwa sababu vyama vyote viwe vya upinzani au tawala lengo lake ni kutaka kuleta maendeleo kwa wananchi wake ili taifa liweze kusonga mbele.

Juzi akiwa jijini Arusha aliendelea kusisitiza kauli yake hiyo kwa kusema kuwa siasa sio uadui na yeye anauchukulia upinzani kama changamoto ya kumwezesha kutimiza wajibu wake ipasavyo.

Tanzania imekuwa ikisifiwa hata na mataifa ya nje kutokana na kuwapo kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa na vile vile utaratibu wa kipindi cha marais kukaa madarakani.

Katika nchi zingine imeonekana zikiingia katika machafuko kutokana na kutoheshimu katiba na wakati mwingine kulazimisha kuibadili ili rais aliyepo madarakani aendelee kutawala badala ya kuwaachia wenzake nafasi ya kuleta mabadiliko.

Wananchi wanaendelea kuwa na imani na Rais Samia, akiwa mama anayewasikiliza watoto wake bila ubaguzi na watapenda kusikia siku hiyo muhimu kwa wanawake anawaambia nini.

Ujasiri ulifanywa na BAWACHA wa kuandaa kongomano hilo ni jambo la kuigwa na wanawake wa vyama vyote. Tunajua rais angependa kusikia kilio cha wanawake wenzake na matatizo wanayopitia hasa katika kusaka nafasi za uongozi kupitia kwenye vyama vyao na hata kwenye sehemu zao za kazi.

Bila shaka BAWACHA watakuwa wamealika wanawake wa vyama vingine kwenye kongamano hilo ili waweze kupata mawazo, uzoefu na changamoto kupitia kwa wenzao.

Rais pia angependa kusikia mawazo tofauti kutoka kwa wanawake wanaotoka kwenye vyama vingine vya siasa ili kufukia hatua nzuri ya kuketi pamoja na kuyafanyia kazi na kuwa na Tanzania yenye wanawake wanaoshirikiana kwa mawazo na vitendo.

**Mungu ibariki Tanzania.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Marundo ya taka kando ya barabara yanatukera

**KUWA** na majiji na miji misafi ndicho kipaumbele cha zama mpya ya Tanzania. Mazingira bora na uhifadhi wa mitaa, barabara, maeneo ya wazi, vyanzo vya maji na kwa ujumla nchi iliyotakata.

Juhudi zimefanyika kuwaondoa wafanyabiashara wanaokwenda kinyume na utaratibu lakini kuwa na kandarasi za kuzoa na kutupa taka kwa wakati ili kuyaacha maeneo ya miji, barabarani na mitaani yakiwa safi.

Tukiangalia suala la taka tatizo bado ni kubwa, kwenye maeneo mengi ikielekea kuleta hatari kwa afya, heshima za miji na hata kikwazo kwa ujio wa watalii na wawekezaji wa kigeni.

Kumekuwapo na mazoea yaliyojengeka ya kuhifadhi taka kando ya barabara wanaofanya hivyo wanazikusanya kusubiria gari la taka, lakini wakati mwingine zinaweza kumaliza hata wiki bila gari kufika eneo hilo.

Ni mambo yanayochangia uchafuzi wa mazingira kuanzia hewa kutokana na harufu mbaya inayokera wakazi jirani na marundo, uzalishaji wa funza, wadudu kama mbu, inzi, maji machafu na wanyama kama panya na kunguru lakini hugeuka makazi ya paka na hata mbwa kwa maeneo mengine.

Wote hao hujikusanya kusaka chakula hasa mabaki ya vyakula na mizoga.

Ikumbukwe kuwa taka zisipohifadhiwa kwenye mazingira salama, zinaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa hasa kipindupindu, kuharisha, kuhara damu na homa ya matumbo.

Hali hiyo inafaa kudhibitiwa kwa serikali kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuhifadhi taka kabla hazijachukuliwa na magari makubwa kwenda dampo badala ya kuzikusanya pembezi ya barabara.

Hali hiyo, itapunguza kero hiyo kwenye jamii zinazoishi jirani na taka kwa kuwa wakati mwingine husababisha njia zisipitike na kuongeza foleni kwenye barabara na hata kusababisha ajali kwa sababu madereva hulazimika kuzikwepa au kupita juu ya marundo hayo na kusambaza zaidi uchafu.

Barabara inafaa kubaki safi ili kupitisha vyombo vya moto na sio vinginevyo, labda kwa dharura na kunatakiwa kuwapo na taarifa kwa watumiaji.

Taka zimezagaa maeneo ya Uswahilini hata katika majiji makubwa kama Mwanza ndiko changamoto ilipo kama wanavyothibitisha wakazi wa maeneo ya Mwananyamala na Buguruni Dar, wakizungumza na vyombo vya habari.

Kadhalika wakazi wa maeneo ya Makoroboi Mwanza nao wana kilio kama hicho, mara nyingi wanalalamikia zimerundikwa barabarani kusubiri magari ya ukusanyaji.

Uswahilini Mwananyamala kwa Mama Zakaria Dar ni mfano, kadhalika Kwa Kopa, Barabara ya Kinondoni maeneo hayo imekuwa kama utamaduni kuwa na taka kila wakati.

Mkazi mwingine maeneo ya Magomeni wilayani Kinondoni Salama Malenda, ana kilio cha taka, akiiomba serikali kulifanyia utatuzi tatizo na kero hiyo anayoona inaiaibisha nchi.

"Wageni wanakuja Tanzania kutalii au kwa malengo mengine ya kibiashara wanapokuta uchafu umerundikwa barabarani hii haileti picha nzuri kwa serikali na wananchi wake, yawezekana si nia ya serikali lakini watumishi wake ndio wanazembea na kulegalega kwenye majukumu yao.

Ni vyema kufanya juhudi na kuiga mfano kwa nchi za wenzetu hasa walioendelea kufanyakazi kwa bidii na kusafisha miji na mazingira yetu ikiwamo kuzoa taka na kuzihifadhi kwa ufanisi ili kuondoa kero.

Juhudi za kuwapanga wafanyabiashara na kuandaa mazingira safi ya miji na majiji ziende pamoja na kuzoa taka na kuzihifadhi bila kuchelewa ili kupunguza kero kwa wananchi ambao pia huchangia gharama za kuondoa taka kwenye makazi na biashara zao.

# Rais Samia alivyoifungua Tanzania utalii wa bahari

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, Machi 14, mwaka huu atazindua boti ya kisasa itakayotumika kwa ajili ya kufanya utalii wa baharini kwenye Bahari ya Hindi.

Upatikanaji wa boti hiyo ni jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, kuhifadhi rasilimali na kukuza utalii nchini, huku serikali ikidhamiria kufikisha watalii milioni tano na kuliingizia taifa pato la Dola milioni sita ifikapo mwaka 2025.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, Waziri Mchengerwa, alisema wakati meli hiyo ikizinduliwa, tayari meli tatu zinatarajia kutia nanga nchini zikiwa na takriban watalii 400 kutoka sehemu mbalimbali duniani wiki hii.

Meli hizo ni pamoja na Corals Geographic Cruise inayotarajia kuingia nchini kesho ikiwa na watalii 120, Le Jaques Cartier-Ponant yenye wageni 105 na Le Jaques Cartier- A & Luxury Expedition itakayoingia nchini Machi 14, mwaka huu ikiwa na watalii 138.

Kuhusu boti hiyo iliyotengenezwa nchini, Mchengerwa alisema ni miongoni mwa boti za kisasa ambayo inamilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), yenye vifaa vya kisasa vya kumfanya mtalii aweze kufurahia safari akiwa ndani.

Alisema boti hiyo imetengenezwa na vioo vyenye lensi maalum vitakavyomwezesha mtalii kuona viumbe mbalimbali baharini hata kama hawezi kuogelea.

Mchengerwa alisema boti hiyo inayofahamika kwa jina la TAWA Sea Cruiser, imetengenezwa na Watanzania wazawa kupitia Kampuni ya Songoro Marine Transport Ltd na ina uwezo wa kuchukua watalii 50 kwa wakati mmoja.

"Tunampongeza na kumshukuru rais kwa kututafutia fedha ambazo zimeweza kununua boti hii ambayo ni ya kiwango cha kimataifa kabisa kwani sasa tuna matarajio makubwa kwamba anakwenda kuifungua Tanzania kwenye utalii wa baharini na tayari watalii wameshaanza kumiminika kuja kujionea vivutio vyetu vya utalii kwa upande wa baharini," alisema Mchengerwa.

Alisema serikali kwa kumiliki boti yake ya utalii itasaidia kuongeza na kukuza utalii wa ndani, wananchi kutoka sehemu mbalimbali nchini watakuja kutembelea na kujionea vivutio mbalimbali ambavyo Tanzania imebarikiwa na ambavyo havipatikani sehemu nyingi duniani.

Baadhi ya vivutio hivyo ni pamoja na viumbe ambao wapo kwenye orodha ya viumbe wa baharini ambao wapo hatarini kutoweka kabisa duniani (CITES) lakini Tanzania wanapatikana.

Viumbe hao ni pamoja na nguva, potwe, kasa na silikanti ambao wote wameonekana katika eneo la bahari ya Tanzania.

"Tanzania inaaminika kuwa na mifumo ya bioanuai nzuri ambayo ina bustani nzuri za matumbawe na aina nyingi za samaki kuliko sehemu nyingi duniani," alisema.

Hadi sasa Tanzania ina maeneo maalum yaliyohifadhiwa kama Hifadhi za Bahari. Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia, Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma mkoani Mtwara na Hifadhi ya Bahari ya Silikanti iliyopo Tanga.

Pia kuna maeneo tengefu 15 yanayomilikiwa na serikali.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella (wa pili kulia), akipokea zawadi maalum kutoka kwa Mkurugenzi wa Bodi ya Exim Tanzania, Irene Mlola, alipotembelea banda la maonesho ya huduma za benki hiyo kwenye maonesho na mkutano wa pili wa wanawake na vijana wafanyabiashara barani Afrika jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jela maisha kumlawiti mwanawe wa miaka minne

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MAHAKAMA ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Namiungo, Tarafa ya Nakaapanya, Mohammed Ngwelekwe (25), kutumikia adhabu ya kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na hatia ya kumlawiti mtoto wake mwenye umri wa miaka minne.

Adhabu hiyo imetolewa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Tunduru, Honorius Kando, baada ya mshtakiwa kukiri kufanya ukatili huo dhidi ya mtoto wake (jina tunalihifadhi), pia kumjeruhi sehemu mbalimbali za mwili wake.

Hakimu Kando alisema mahakama yake inamhukumu kutumikia adhabu hiyo baada ya kujiridhisha bila kutia shaka kuwa mtuhumiwa huyo alifanya kosa hilo, pia yeye mwenyewe kukiri kutenda ukatili huo dhidi ya mwanawe.

Alisema kitendo kilichofanywa na mshtakiwa huyo kimemfanywa dhidi ya mtoto mdogo na adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha maisha jela.

Awali wakimsomea mashtaka hayo, Mwendesha Mashtaka, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Stephen Msongaleli na Inspekta Machiya Ernest Nangi, mbele ya Hakimu Kando, walidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Februari 24, mwaka huu.

Walidai kuwa mshtakiwa huyo alikabidhiwa mtoto huyo na mtalaka wake, Sofia Mkwanda, Julai mwaka jana baada ya kufikia makubaliano kuwa atamtunza.

Walidai kuwa katika shauri hilo namba 50/2023, shtaka la kwanza ni kulawiti ambalo ni kinyume cha kifungu cha Sheria Namba 254 (1)(a) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Kwa mujibu wa waendesha mashtaka hao, shtaka la pili ni kujeruhi ambalo kinyume na kifungu cha Sheria Na. 225 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejea mwaka 2022.

Baada ya mahakama hiyo kumtia hatiani mshtakiwa huo, waendesha mashtaka hao kwa pamoja waliiomba itoe adhabu kali kwa mtuhumiwa ili liwe fundisho kwa watu wengine ambao wamekuwa na tabia za aina hiyo.

Akitoa utetezi mbele ya hakimu huyo, mshtakiwa huyo aliiomba mahakama kumpatia adhabu ndogo kwa vile hilo ni kosa lake la kwanza, anategemewa na wazazi na mtoto huyo.

Nje ya mahakama, babu wa mtoto huyo na baba wa mshtakiwa, Saudi Gwelekwe, alidai tukio hilo limeleta fedheha kwa ukoo wao, hivyo uamuzi wa mahakama ni stahiki kwa mwanawe. Alidai kuwa mshtakiwa alizaliwa mwaka 1998 na alilelewa kwenye Kituo cha Kulelea Watoto Yatima cha Kanisa la Biblia Tanzania Kituo cha Mbesa Mission baada ya mama yake mzazi kufariki dunia muda mfupi baada ya kujifungua.


Alidai kuwa alikaa kituoni huko kwa miaka minne kisha alikwenda kumchukua na kumlea akiwa nyumbani hadi alipofikia umri wa kujitambua na kuhamia kwenye mji wake akiwa mtu mwema.

Gwelekwe alidai haelewi mahali ambako kijana wake alijifunza tabia hizo za kinyama.

Bibi wa mtoto huyo, Stawa Selemani alidai mjukuu wake alikutwa akiwa na vidonda sehemu mbalimbali za mwili wake, hivyo walimpeleke hospitalini kwa ajili ya matibabu.

Alidai kuwa wakiwa huko ndipo wakagundua mtoto huyo alikuwa anashindwa kuzuia haja kubwa kutoka, hali iliyoonesha alifanyiwa ukatili na walipomhoji, alieleza kuwa amekuwa akiingiliwa na baba yake kwa kipindi kirefu, hivyo wakaamua kuliripoti suala hilo kituo cha polisi kwa ajili ya hatua za kisheria.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



# Halotel, Kisutu, MOI kuadhimisha Siku ya Wanawake uchangiaji damu

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Halotel imeungana na Shule ya Sekondari Kisutu pamoja na Taasisi ya Mifupa (MOI), kuandaa tukio la uchangiaji damu kwa hiari kuelekea Siku ya Wanawake Duniani kesho.

Tukio hilo lilifanyika jana na kujumuisha wadau kutoka taasisi mbalimbali ikiwamo zaidi ya shule 40 zikiwa na wanafunzi 2,000 kutoka mkoa wa Dar es Salaam.

Akizungumza wakati akikabidhi vifaa kwa ajili ya kufanikisha tukio hilo, Mkuu wa kitengo cha Masoko Halotel, Sakina Makabu, alisema lengo ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuokoa maisha ya wagonjwa wenye uhitaji wa damu.

"Kuelekea Siku ya Wanawake Duniani, Halotel imeona ni muhimu kusherehekea siku hiyo kwa kuchangia katika sekta ya afya katika kuunga mkono juhudi za serikali kuboresha sekta hiyo kwa maendeleo ya nchi," alisema Makabu.

"Halotel kwa kushirikiana na MOI imewezesha utekelezaji wa kampeni ya uchangiaji damu chini ya Shule ya Sekondari Kisutu kwa kuchangia vifaa mbalimbali ikiwamo nguo, chakula, vinywaji na vitafunwa kwa ajili ya kutumika wakati wa uchangiaji damu katika viwanja vya Shule ya Sekondari Kisutu."

Alisema wanaamini kufanya hivyo kunasaidia kuipunguzia serikali mzigo wa ukosefu wa damu ya kutosha kuokoa maisha ya wagonjwa katika Taasisisi ya MOI na Hospitali ya Muhimbili.

"Wajawazito, manusura wa ajali, watoto chini ya miaka mitano wapo katika kundi lenye uhitaji mkubwa wa damu, hivyo kufanikisha hili ni ishara ya upendo wa kampuni kwa Watanzania ambao pia ni wateja wake."

Pia alisema sera ya kampuni hiyo sio kibiashara pekee bali pia ni kusaidia jamii, kurudisha sehemu ya faida ili kusaidia serikali kuboresha sekta ya afya na elimu.

Ofisa Habari wa MOI, Patrick Mvungi, alisema wamefurahishwa na mwitikio kutoka kampuni hiyo kwa kuwezesha kampeni ya shule ya sekondari Kisutu ya uchangiaji damu.

"Hii inaonyesha namna kampuni inavyojali afya za wananchi na juhudi zinazofanywa na serikali katika kuboresha sekta ya afya. Ni hatua kubwa kwetu kuelekea kuimarisha zaidi uhusiano wetu na kampuni hii katika kuboresha sekta ya afya," alisema Mvungi.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kisutu, Chiku Mhando, aliishukuru Halotel kwa kuwa mdhamini wa tukio hilo na kuwaomba watu binafsi, kampuni na taasisi mbalimbali kujitokeza kuunga mkono uchangiaji huo ili kuongeza kiwango cha damu kwenye benki ya damu.



Mkuu wa Kitengo cha Masoko Halotel, Sakina Makabu, akikabidhi vifaa mbalimbali kwa Mkuu wa Shule ya Wasichana Kisutu, Chiku Mhando, kwa ajili ya kutumika wakati wa uchangiaji damu jana katika viwanja vya shule hiyo. Katikati ni ofisa kutoka MOI, Joel Mushi na wanafunzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHAVITA yaomba kushirikishwa afya

**Na Hamisi Nasri,** NANYUMBU

CHAMA cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), tawi la Mkoa wa Mtwara, wameiomba serikali kupitia sekta ya afya, kushirikisha watu wenye ulemavu, hasa viziwi katika masuala ya afya ili kundi hilo liwe na uelewa wa kutambua umuhimu wa huduma za afya.

Pia kinawaomba madaktari nchini kuanzisha daftari maalum la kuorodhesha majina ya viziwi wanaokwenda kupata huduma za afya kwenye vituo vya kutolea huduma hizo ili kutambua mwamko wa viziwi na idadi ya viziwi wanaokwenda na kupatiwa huduma za afya.

Ombi hilo lilitolewa juzi wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara na Katibu wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Mkoa wa Mtwara, Kassimu Mchindula, aliposoma taarifa ya chama hicho katika kongamano la ushawishi kuhusu ushiriki wa viziwi katika masuala ya afya lililofanyika Shule ya Sekondari Managaka iliyoko wilayani hapo.

Alisema kongamano hilo linafanyika chini ya mradi unaolenga kutoa elimu ya afya ya uzazi na haki za uzazi kwa wanawake na vijana viziwi ili kundi hilo litambue vya kutosha masuala ya afya ya uzazi na kushiriki kikamilifu, ikiwamo kuhudhuria kwenye huduma za afya kwa wakati.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Shirika la Bills Foundatiton, una malengo mahususi ya kuhamasisha na kuwashawishi watendaji wa serikali wa sekta ya afya wakubali kuwashirikisha viziwi kwenye masuala ya afya ili kujenga uelewa wa pamoja katika masuala hayo ya msingi.

Alisema watendaji wa sekta ya afya wanapaswa kuwa mfano bora katika kushirikiana na viziwi katika masuala ya afya na haki za uzazi kwa kutoa huduma kwa viziwi kwa kuzingatia hali zao bila kuwabagua.

Mchindula alisema iwapo kundi hilo la viziwi likishirikishwa ipasavyo katika kushiriki kwenye mambo ya afya, kutakuwa na mwamko chanya kwa kundi hilo kutambua umuhimu wa huduma za afya, ikiwamo kuhudhuria kliniki kwa wakati na kutumia dawa kwa usahihi.

Alisema faida nyingine ya kuwashirikisha viziwi katika masuala ya afya ni kuwasaidia kuwa na mwamko wa kutumia huduma za afya pamoja na kufuatilia haki zao za msingi katika kupata huduma za afya kwa wajawazito.

Awali akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, Mariamu Chaurembo, alisema serikali itaendelea kuwashirikisha watu wenye ulemavu, hususan viziwi katika mambo yote ya maendeleo ikiwamo ya afya.

Alisema serikali mara zote imekuwa ikishirikisha watu wenye ulemavu pamoja na kutambua thamani yao na ndio maana Wilaya ya Nanyunbu imeshatoa mikopo mbalimbali kwa watu wenye ulemavu ili wajiendeleze kiuchumi.

# Norway yaridhishwa na huduma Benjamin Mkapa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BALOZI wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, ameridhishwa na huduma za afya zinazotolewa na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kati ya Benjamin Mkapa (BMH) jijini Dodoma.

Elizabeth aliyefika hospitalini huko, akiambatana na ujumbe wa watu 23 kutoka ubalozini, alieleza kuridhishwa na huduma hizo, pia akitembelea miradi inayotekelezwa jijini Dodoma ili kujiridhisha na tamko la serikali kwa mabalozi kuanza kuhamia makao makuu ya nchi.

"Huduma zenu ni nzuri na tumeona vifaa vya kisasa kwenye baadhi ya vyumba wanavyolazwa wagonjwa, wakiwamo viongozi," alisema Elizabeth.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweli, alimhakikisha balozi huyo kuwa serikali imefanya uwekezaji mkubwa hospitalini huko, ikiwamo kuongeza huduma na vifaa tiba vya kisasa ili kuiwezesha kuwahudumia viongozi wa ngazi zote, wakiwamo mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini.

"Kuna vifaa kama MRI na CT-Scan, matoleo ya kisasa, kuna mradi wa kituo cha mionzi tiba na huduma nyinginezo kama unavyojionea," alisema Shekimweli.

Aliwataka mabalozi hao kutokuwa na wasiwasi wowote kuhusu huduma za afya ambazo zinatolewa na wataalamu wa afya kwenye hospitali hiyo.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika alitoa taarifa fupi kuhusu huduma zinazotolewa na hospitali hiyo zinazojumuisha huduma zote za kibingwa.

"Tunatoa huduma nyingi za ngazi ya kibingwa na ubingwa bobezi, ikiwa ni pamoja na huduma za kupandikiza figo, huduma za magonjwa ya moyo kwa kutumia maabara maalum ya uchunguzi na matibabu ya moyo na huduma za upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu," alieleza Dk. Chandika.

Alisema Hospitali ya Benjamin Mkapa inaendelea kupanua huduma zake huku ikipanga kujenga kituo cha matibabu ya moyo, kituo cha upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo, mifupa, Kituo cha Mama na Mtoto na Kituo cha Magonjwa ya Dharura.

"Miongoni mwa mipango ya baadaye ni kujenga kituo cha tiba za upandikizaji wa viungo," alisema Dk. Chandika.

## TEA, TAHA yanufaisha vijana 400 kilimo bustani

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

VIJANA zaidi ya 400 wamenufaika na mafunzo ya kuendeleza ujuzi kwenye sekta ya kilimo yaliyofadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na kuendeshwa na Taasisi ya Kilimo-Biashara cha Bustani na Mboga (TAHA).

Katika kuunga mkono jitihada za serikali, TEA ilitoa ruzuku ya Sh. milioni 130 kwa TAHA kwa ajili ya mafunzo ya kuendeleza ujuzi katika sekta ya kilimo kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) mwaka 2021.

Kiongozi wa uzalishaji TAHA, Gilliad Daniel, alisema mwishoni mwa wiki kuwa kupitia ruzuku ya SDF vijana 437 wamenufaika na mafunzo hayo ambayo yalifanyika katika maeneo mbalimbali ya jijini Arusha.

Mafunzo hayo yalitolewa na Taasisi ya TAHA na hadi sasa asilimia 90 ya vijana hao ni wakulima wakubwa wa mboga na matunda wanaofurahia soko la ndani na nje ya Tanzania.

Alisema ruzuku waliyopewa kupitia (SDF) imeleta mabadiliko chanya ndani ya taasisi yao kupitia programu ya kuendesha mafunzo ya kuwajengea vijana uwezo katika kilimo cha bustani baada ya mwitikio kuwa mkubwa tofauti na walivyotarajia.

Alisema TEA ilitoa ruzuku kwa TAHA kupitia SDF kwa lengo la kufadhili mafunzo ya ujuzi kwa vijana katika sekta ya kilimo kama moja ya sekta za kipaumbele.

Alisema takwimu na machapisho mbalimbali yamekuwa yakionyesha kuwa asilimia 90 ya ardhi ya Tanzania hulimwa na wakulima wadogo na sekta ya kilimo inatoa ajira kwa asilimia 65.5 na inachangia asilimia 29.1 ya pato la taifa, asilimia 30 ya soko la nje na asilimia 65 ya malighafi za viwandani.

**Mafunzo hayo yalitolewa na Taasisi ya TAHA na hadi sasa asilimia 90 ya vijana hao ni wakulima wakubwa wa mboga na matunda wanaofurahia soko la ndani na nje ya Tanzania.**

# Watumishi h'shauri, wakuu wa idara wachunguzwa ubadhirifu mamilioni

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WATUMISHI 12 wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido mkoani Arusha, wakuu wa idara nne walioshushwa vyeo, wameamriwa kukaa kando kupisha uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa zaidi Sh. milioni 150.

Kwa mujibu wa Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wilayani humo, Solomoni Lekui, watumishi hao kwa sasa hawaruhusiwi kujihusisha na kazi yoyote.

Alisema ubadhirifu kwa watumishi hao, ulifanyika kinyume na utaratibu kwa kuwa walitumia vibaya madaraka yao walipokuwa kazini, hivyo ameomba mamlaka husika kuchukua hatua dhidi yao ili iwe fundisho kwa wengine.

Alisema chama hicho kiko katika mchakato wa kusimamia, kuelekeza na kukemea watumishi wanaokwenda kinyume na utaratibu kwa kuwa kamwe hawataweza kukaa kimya kuangalia mambo yakienda ovyo.

"Tunaomba mamlaka husika ziweze kuwachukulia hatua wale wote waliotajwa katika ripoti hiyo kwa madai ya ubadhirifu wa mamilioni ya pesa Longido,"alisema Lekui.

Aidha, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Saimon Oitesoi, alipoulizwa kuhusu amri hiyo kutolewa na CCM, alidai kuwa uamuzi huo umefikiwa baada ya kufanyika kwa uchunguzi wa taarifa ya ukaguzi ya mwaka 2021.

Vilevile Mkurugenzi wa Halmashauri ya Longido, Stephen Ulaya, alisema hatua za awali zimeshachukuliwa kwa wakuu wa idara nne kushushwa vyeo na kupangiwa kazi nyingine na hatua zingine zitafuata baada ya uchunguzi kukamilika.

Mkurugenzi huyo alitaja wakuu wa Idara walioshushwa vyeo ni pamoja na idara ya ugavi na ununuzi, ujenzi, mapato na biashara na wamepangiwa kazi nyingine.

Alisema watumishi wengine ambao wanadaiwa kutuhumiwa na ubadhirifu, matumizi mabaya ya ofisi na ukiukwaji wa utaratibu uchunguzi bado unaendelea na ikibainika hatua zaidi zitachukuliwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Longido, Saimoni Oitesio, alipoulizwa juu ya ubadhirifu huo, kwa nini ameshindwa kusimamia alisema kushindwa kusimamia siyo kweli kwa kuwa yuko kwa ajili ya kulinda fedha za umma bila kumwonea mtumishi yeyote.

Alisema kutokana na umakini wake wa usimamizi umesababisha baadhi ya wafanyakazi kusimamishwa kazi na wengine wametolewa katika kuongoza idara hiyo na wako wanaochunguzwa kwa madai ya kula fedha za umma. Kuhusika madai ya kuchukua zabuni kupitia gari yake binafsi, mwenyekiti huyo, alisema siyo kweli kwa kuwa gari lake alilikodishia kwa mtu binafsi kufanya kazi ya halmashauri, siyo yeye amefanya kazi hiyo, kama inavyodaiwa na watu wanaosambaza taarifa kwenye mitandao ya kijamii.

Alisema aliikodisha gari hilo mwaka jana kwa mtu binafsi na siyo mwaka huu na kwa kipindi cha mwaka gari hilo lilikuwa limepaki nyumbani kwake.

Alisema watumishi wa halmashauri watakuwa marafiki endapo watazingatia sheria na taratibu na tofauti na hapo hatawaacha salama hasa wanaokula fedha za umma kwa kuwa atashughulika nao ipasavyo.



Wanawake kutoka makanisa ya Anglikana, Romani Katoliki na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania KKKT Muheza mkoani Tanga, wakiwa kwenye maandamano ya amani kuadhimisha Siku ya Maombi ya Mwanamke ambayo hufanyika kila mwaka duniani, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kesi inayomkabili Mnyeti na wenzake kusikilizwa Machi 20

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

KESI ya madai inayomkabili Mkuu wa Mkoa wa zamani wa Manyara, Alexander Mnyeti, itatajwa tena katika Mahakama Kuu Kanda ya Manyara, Machi 20, mwaka huu.

Siku hiyo mahakama itaketi kwa ajili ya kusikiliza kikao cha kwanza kitakachoandaa utaratibu wa mwenendo wa kesi.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Manyara, John Kahyoza, alisema mahakama hiyo ilikaa kupitia malalamiko ya wadai na majibu ya wadaiwa, ambayo yalikuwa kwenye amri iliyotolewa Februari 2, mwaka huu.

Mdai katika shauri hilo ni Kampuni ya Uwindaji ya HSK Safaris Ltd, iliyopo Wilaya ya Simanjiro.


Wadaiwa katika shauri hilo ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Emboreet, Belinda Sumari na Salehe Alamry.

Mdai ambaye ni Kampuni ya HSK Safaris Ltd, anawakilishwa na Wakili Edmond Ngemela, wakati mdaiwa wa kwanza (Mnyeti) anawakilishwa na Wakili Kuwengwa Ndejekwa.

Mdaiwa wa pili (Sumari), hana wakili na mdaiwa wa tatu anawakilishwa na Wakili Sheki Mfinanga.

Katika kesi hiyo Mnyeti anadaiwa kushirikiana na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Emboreet, Sumari na Salehe Alamry kuinyang'anya Kitalu cha Uwindaji, Kampuni ya HSK Safaris Ltd, bila kufuata sheria.

Kwa mujibu wa Wakili wa Kampuni ya HSK Safaris Ltd, Ngemela, mdaiwa wa kwanza na wa pili, walitumia madaraka yao vibaya na hivyo kusababisha wadai kupata hasara ya zaidi ya Sh. bilioni moja.



# RC Shigela awataka TRA kuacha kuwababambikia kodi w’biashara

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, ameitaka Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), mkoani humo kuacha kuwabambikia kodi wafanyabiashara wakiwamo wawekezaji katika sekta mbalimbali.

Shigela amesema hatua hiyo itasaidia kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa mkoa huo na kuongezeka kwa mapato ya serikali.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua hoteli iliyopo mtaa wa Nyankumbu Mjini Geita inayomilikiwa na mwekezaji mzawa, Jackson Dalushi.

Alisema serikali haitaki kuona wafanyabiashara wakitishwa, kuombwa rushwa na kutozwa kodi isiyostahili na kwamba vyombo vya usalama vitashughulika na watakaokwenda kinyume cha maelekezo hayo.

“Serikali hii inataka watu wafanye biashara bila kunyanyaswa kwa kuombwa rushwa, kutishwa na kutozwa kodi kubwa zisizostahili,” alisema Shigela.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornery Magembe, alisema serikali inatambua umuhimu wa wawekezaji wa ndani na nje kwa kuwa wanasaidia kuongeza ajira kwa vijana na mapato kwa halmashauri.

Meneja wa hoteli hiyo, Salmu Kalanje alisema ujenzi wake ulianza mwaka 2012 na kukamilika 2023.

Kadhalika, aliomba serikali kudhibiti uharibifu wa barabara inayopita katika mradi huo pamoja na uchafuzi wa taka ngumu ombi ambalo lilipokelewa na Mkuu wa Mkoa na kuahidi kulishughulikia kupitia Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA).



Askofu wa Jimbo la Nyanza Ukanda wa Dhahabu, Enock Sando, akitoa neno kwenye ibada katika Kanisa la Waadventista Wasabato Shinyanga Mjini juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Vikundi 212 kuburuzwa kortini kwa kushindwa kufanya marejesho

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga inatarajia kuvifikisha mahakamani vikundi 212 vya wajasiriamali ambavyo vinadaiwa Sh. milioni 819.8 walizokopeshwa.

Vikundi hivyo vilikopeshwa fedha hizo ili kufanyabiashara kwa masharti ya kurejesha mikopo hiyo lakini vimeshindwa kufanya hivyo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Robert Kwela, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu vikundi vilikopeshwa fedha kuanzia mwaka 2018 hadi 2021.

Alisema vikundi vya ujasiriamali 212 vinatarajiwa kufikishwa mahakamani hivi karibuni na kati ya hivyo 71 ni vya vijana, wanawake 133 na watu wenye ulemavu ni vikundi vinane.

Hivyo, alivitaka kufanya marejesho haraka ili kuvipatia fursa vikundi vingine kukopa na kukuza mitaji yao vinginevyo vitafikishwa mahakamani.

Aidha, alisema mwaka wa fedha 2018/2019 vikundi 60 vilikopeshwa na kati ya hivyo 24 vilikuwa vya vijana ambavyo vilipewa Sh. milioni 41.9, wanawake 34 (Sh. milioni 47.24) na vikundi viwili vya watu wenye ulemavu vilikopeshwa (Sh. milioni 2.68).

Kadhalika, alisema mwaka wa fedha 2019/202 vikundi 58 vilikopeshwa na kati ya hivyo 16 vilikuwa vya vijana ambavyo vilikopeshwa Sh. milioni 54.249, wanawake vikundi 40 Sh. milioni 51.534 na viwili vya watu wenye ulemavu vilipewa Sh. milioni 2.667.

Kwela aliongeza kuwa mwaka wa fedha 2020/2021 vikundi vya ujasiriamali 94 vilikopeshwa na kati ya hivyo vya vijana vilikuwa 31 vilivyokopeshwa Sh. milioni 292, vikundi 59 vya wanawake vilikopeshwa Sh.milioni 309 na vikundi vinne vya watu wenye ulemavu vikikopeshwa Sh. milioni 18.54.

“Vikundi vyote hivi havijafanya malipo yao kwa muda uliopangwa na hivi karibuni tutaandaa mashtaka kwa kushirikiana na mwanasheria wetu wa halmashauri na tutavifikisha mahakamkani,” alisema na kuongeza:

“Vikundi hivyo vinatakiwa kurejesha mikopo hiyo ili kuvipatia fursa vikundi vingine kukopa kwa sababu fedha hizi ni za umma na siyo za watu binafsi”.

Mkazi wa Mtaa wa Nyakato, Kata ya Nyasubi, Glory Samweli, alisema baadhi ya vikundi vya ujasiriamali vikipewa mikopo havina shughuli maalumu badala yake wakizipata wanagawana na kufanya mahitaji ya familia na hivyo ukifika muda wa marejesho wanashindwa.

Alisema vikundi vingi vimekuwa vikijificha kwenye ufugaji wa mifugo na kutoa mfano wa kikundi kimoja cha wanawake wa Kata ya Majengo kilijificha kwa ufugaji wa mradi wa nguruwe na kilipopata fedha wanachama wake waligawana na mradi ukafa.

Mkazi mwingine, Sodoka Wilisoni, alisema kabla ya vikundi hivyo kupewa fedha vinatakiwa kupewa elimu ya biashara kulingana na shughuli wanazozifanya na wawe wanapewa kwa awamu.

# Wazazi waonywa kutumia lugha ya matusi kwenye malezi

**Na Titus Mwombeki,** KAGERA

WAZAZI mkoani Kagera wametakiwa kuacha kutumia lugha za matusi wakati wakitekeleza jukumu la malezi na makuzi kwa watoto wao.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Elimu Michezo, Khefa Elias, kwa niaba ya Ofisa Maendeleo ya Jamii mkoani Kagera wakati wa warsha maalumu iliyoandaliwa na Shirika la TADEPA.

Warsha hiyo ilihusisha waandishi wa habari na ililenga kuwajengea uwezo juu ya programu ya taifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

“Tabia za namna ya ndoa zilivyo kwa sasa unamkuta baba anampiga mama na anamtolea maneno ya matusi hususani akiwa mjamzito, tunatakiwa kujua kuwa makuzi ya mtoto yanaanzia tangu akiwa tumboni mwa mama yake yaani kuanzia miaka 0-8,” alisema.

Aliongeza: “Hivyo kama mnapigana au kugombana nyumbani maana yake mtoto anajifunza kule tumboni anajua kinachoendelea na hata atakapokuwa amezaliwa usishangae kuona yale mliyokuwa mkiyafanya akiwa tumboni anayaiga na kuyafanya katika makuzi yake”.

Aidha, alisisitiza kuwa athari ya malezi yasiyozingatia maadili yamekuwa yakisababisha kutokea kwa masuala mbalimbali ya unyanyasaji yakiwamo ya mauaji huku akiwasihi wazazi kuepuka kutatua masuala ya ndoa mbele ya watoto wao.

Ofisa Mradi wa Mtoto Kwanza kutoka TADEPA, Abmeleck Richard, aliomba serikali kuwekeza kwa watoto wadogo hususani waliopo darasa la awali kwa kuwajengea miundombinu wezeshi ikiwamo madarasa mazuri ya kujifunzia.

“Serikali imekuwa ikijitahidi sana katika tatua matatizo yanayowakumba wananchi wake ila kwa bahati mbaya unakuta mtoto bado hajapewa kipaumbele, chukulia mfano sasa hivi serikali inajenga madarasa mengi katika shule ila huwezi kuona imeweka nguvu kwenye madarasa ya watoto wa awali,” alisema.

Alisema nguvu nyingi zinawekwa kwa wanafunzi ambao wanatarajia kufanya mitihani kwa maana ya kuanzia darasa la nne hadi la saba.

Nipashe
TESA
Jumanne Machi 7, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

VITA VYA RUSSIA Vs UKRAINE
Ushindi wake uliko, ni zaidi ya teknolojia, silaha kali za kisasa



Ukurasa 12

Acheni kutumia simu kuonyesha familia zikila chakula sebuleni



Ukurasa 13

**Fahamu sababu mwanao kumaliza shule pasipo kujua chochote, hata 'a'**

ELIMU

**NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA**

SKENDO KWA FAMILIA

# Ni pale baba alipogeuka mume kwa mama na binti

- •Mlezi huyo adaiwa kumpa mimba mwana anayemlea
- •Aachishwa shule jicho labaki polisi, mahakama

WAKATI kinamama wanajiandaa kushangilia na kuifurahia Siku ya Wanawake Duniani, zipo familia zina machungu kutokana na mama pamoja na mabinti zake kudhalilishwa kingono na wenza wa ndoa.

Kunyanyaswa huko kunafanywa na baba mlezi au wa kambo, ambaye licha ya kufahamishwa kuwa ni mtoto wa mkewe ambaye amekubali kumlea baada ya kufunga ndoa na mama yake, mwanaume huyu anaamua kumdhalilisha binti wa kufikia.

Wanawake wanakumbushwa kuwa mtoto wa kike ni mawindo ya baba wa kambo au walezi, japo ni wenza wa ndoa wanaoishi nao.

Ni ushauri unaotolewa na mama ambaye binti yake leo ni mjamzito baada ya kupewa mimba na baba mlezi, mkasa unaotokea mkoani Pwani Kijiji cha Visiga Madafu.

Anasema ni mume au mwenza wake, ambaye binti huyo anamwita baba mlezi au baba wa kambo na kwamba binti huyo ni mwanafunzi wa Sekondari ya Visiga ambaye alitakiwa kuwa kidato cha pili.

Amekwambishwa kimasomo na baba wa kumlea aliyembaka na kumpa ujauzito wakati mama yake akiwa mashambani.



Ndivyo mabinti wanavyokuwa mawindo ya baba mlezi baada ya mama kufunga ndoa. **PICHA: MTANDAO**

**MAELEZO YA BINTI**

"Nilikosa ujasiri wa kukataa mambo haya niliyolazimishwa na baba. Nilipata hofu nilikuwa namwogopa sana mama hata nikashindwa kumwelezea ninachofanyiwa," anasema msichana huyo anapozungumza na Nipashe.

Akiwa mwanafunzi wa kidato cha pili katika Sekondari ya Visiga, anakatishwa masomo na baba yake huyo baada ya kupimwa na kugundulika kuwa ni mjamzito mwezi Februari mwaka huu.

Vipimo vinafanyika shuleni jambo ambalo lilimfadhaisha kwa vile alikuwa haweza kulalamika na kueleza kile kilichokiita udhalimu aliokuwa anaofanyiwa na baba yake wa kufikia.

Akizungumza na Nipashe anasema akiwa kidato cha kwanza Machi mwaka 2022 baba mlezi alianza kumnyanyasa kingono na alishindwa kumweleza mama yake kutokana na vitisho na hofu.

"Siku moja mama na ndugu zangu waliondoka kwenda shamba, baba yangu pia aliongozana nao akiwa kwenye baiskeli akiwabebea chakula na maji, niliachwa nyumbani peke yangu bila chakula," anaeleza.

Aliamua kupika chakula ili asishinde na njaa kwa vile kulikuwa na mboga na unga na kwamba wakati anaendelea kupika, ghafla baba alirejea nyumbani na kumuuliza kwanini anapika chakula na kula mwenyewe bila maelekezo ya mama?

"Nikamwelezea kuwa mama hakuniachia chakula cha mchana, akaendelea kunifokea na huku akiniambia nitamwambia mama yako mambo haya unayofanya."

Anasema alimuomba radhi asimweleze mama yake kuhusu alichokifanya badala yake alijibiwa kuwa amesamehewa lakini sio moja kwa moja.

"Baba aliingia chumbani akaniita akifoka bila kutarajia alinishika, kunibana na kunizidi nguvu kuanzia wakati huo Machi 22, amekuwa akinivizia kwa kila namna na kila mwanya anaoupata kunitumia kila anapotaka na kunitishia kila nikikataa. Madai yake ni kumweleza mama kuwa najipikia chakula cha peke yangu na kula mwenyewe kwa siri," anaeleza.

Anasema hali hiyo ilimchosha lakini baba yake alikuwa akimvizia akifanya hivyo nyumbani wakiwa wamebaki wawili na wakati mwingine akiwapo mdogo wangu anamtuma dukani mbali ili nibake mwenyewe na kuninyanyasa ananiita akiona nimekataa ananifuatа nilipo tena ananitishia na amekuwa akinifanyia unyanyasaji chumbani kwake na mama yangu," anaeleza.

Anatamani kusoma na kufanikiwa zaidi akisema: "Bado ndoto yangu ni kusoma kuendelea na masomo na hata mama yangu ameniahidi baada ya kujifungua nitarudi darasani."

**MIMBA KUGUNDULIKA**

Mama mkubwa wa binti huyo Anna Ulomi anaeleza kuwa alipigiwa simu na mdogo wake ambaye ni mama wa mwanafunzi huyo, akimwomba kwenda shuleni kusikiliza wito kutoka kwa mwalimu mkuu na kufahamishwa sababu ya kusimamishwa masomo binti yao.

Anasema anaitikia wito wa kwenda sekondari Visiga anapoelezwa kuwa tatizo alilonalo binti huyo ni mjauzito na ndipo aliporudi nyumbani kufanya mahojiano ya kina kumjua aliyempa mimba.

"Mwalimu ananiambia amemhoji mno kuhusu aliyempa ujauzito lakini alitaja watu tofauti. Tulipofika nyumbani kwangu nilimhoji sana alikuwa kimya niliamua kutumia

INAENDELEA UK.12

ELIMU

**SABATO KASIKA, BAGAMOYO**

KINAMAMA WAFUNZWA TEHAMA NA KUAMBIWA...

# Acheni kutumia simu kuonyesha familia zikila chakula sebuleni

WANAWAKE ndiyo wachangiaji wakuu wa maendeleo kuanzia kilimo, ufugaji, biashara, malezi ya watoto hata huduma kwa wagonjwa ingawa pamoja na mchango huo, wanagubikwa na kazi nyingi za kifamilia na kijamii bila malipo.

Majukumu yanavyowazidia ni kwa nadra hupata nafasi ya mafunzo ya mambo mbalimbali yanayoendelea katika jamii, hivyo kuendelea kuwekwa nyuma kimaendeleo ni kwa mujibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambacho kinasema Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ni nyenzo na fursa ya kujiendeleza ili waweze kuchangia maendeleo yao na jamii zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, anasema kwa kutambua umuhimu huo, wameratibu mafunzo ya TEHAMA kwa wanawake wajasiriamali zaidi ya 300, wanatoka katika vikundi mbalimbali wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, wakifunzwa wakati huu wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Jumatano Machi 8.

Kaulimbiu ni "ubunifu na mabadiliko ya teknolojia, chachu kuleta usawa wa kijinsia," ukweli ni kwamba ni asilimia chache kati yao wanaomiliki simu au kuwa na uelewa kuhusu mambo ya dijitali, hivyo suala la kupata elimu kuhusu teknolojia ni la muhimu kwa mwanamke, katika dunia ya leo," anasema Anna.



Kinamama wajasiriamali wakionyesha bidhaa baada ya kujifunza jinsi ya kutumia simu ili kuboresha biashara zao. **PICHA: SABATO KASIKA**

Anawataka wawe chachu ya kupinga vitendo vya unyanyasaji vinavyowabagua na kuvunja haki zao za msingi na kwamba maadhimisho hayo yanakuja huku dunia ikiwa katikati ya maendeleo ya teknolojia ya kielektroniki ambayo kwa kiasi kikubwa yamewaacha nyuma kuanzia biashara wanazofanya, kujifunza na kuitumia kwa tija.

Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa, katika karne hii ya 21, biashara na matangazo yanategemea teknolojia, na kwamba watu wanaishi katika ulimwengu wa dijitiali, kila kitu hakina budi kufanywa kidijitali.

"Unaweza kuwa na biashara au kampuni inayotoa huduma au bidhaa imara, lakini usipotumia bidii kujitangaza ama kujiweka 'online', unaweza kuzidiwa na watu ambao huduma zao hazina ubora zaidi yako," anawaambia washiriki na kuongeza kuwa kujitangaza kimtandao ni njia rahisi na isiyo gharama kuwafikia watu wengi zaidi na wasipofanya matangazo ya biashara wafanyazo zitaishia kwa watu wachache wanaowazunguka.

Mkurugenzi Mtendaji anaongeza kuwa, kwa watu walioendelea, siku hizi wakitaka msaada wa jambo fulani, hatua ya kwanza ni kushika simu na kuperuzi kuhusu wakitakacho. Hapo ndipo huweza kukutana na majibu ya masuala wanayoyataka mtandaoni.

"LHRC inataka wajasiriamali wadogo wa Bagamoyo nao wafikie hatua hiyo, nasi tutaendelea kushirikiana na serikali ili elimu ya digitali isambae zaidi," anasema Anna akiongeza kuwa hatua hiyo itasaidia kusukuma gurudumu la ukombozi wa mwanamke, katika nyanja zote, ili kufikia usawa wa kijinsia.

Mtaalamu wa TEHAMA kutoka kampuni ya Digmap Africa, Getrude Mligo, anawafundisha wajasiriamali hao jinsi ya kutumia simu ya mkononi kutangaza biashara zao badala kuweka mambo yasiyo na umuhimu, akisema: "Simu hizi hasa ya 'tachi', zina mambo mengi, ikiwamo sehemu ya kutangaza biashara na zinaelekeza pia jinsi ya mjasiriamali kuwa na ubunifu."

Getrude Mkurugenzi wa kampuni hiyo, anasema kujitangaza mitandaoni hakuna gaharama nyingine mbali na fedha unayotumia kununua vocha.

"Cha msingi ni kujifunza mbinu za uendeshaji na kuchagua njia ipi inakufaa zaidi, lakini baadhi ya wanawake mnatumia vibaya mitandao," anasema Getrude na akieleza kuwa baadhi hutukana wenzao, kuweka watoto wao au familia ikiwa sebuleni, mezani na mengine yasiyo na tija.

"Kwa mtindo huo hamuwezi kufika mbali, katika biashara zenu, tumieni fursa hiyo ya mitandao kutangaza bidhaa zenu mnazozalisha, si vinginevyo, karibia kila mtu yuko facebook au Instagram, ni rahisi watu wengi kuona bidhaa zinazotangazwa humo. Soko liko huko, kwa sababu ndiko wateja waliko. Hivyo kupelekeni biashara zenu fungueni akaunti kwa majina ya biashara mjitangaze," anashauri.

Aidha, anasema mitandao ya kijamii ni watu na kwamba wanataka kufahamu namna ya kuishi na watu ikiwa ni pamoja 'kuposti' bidhaa zao kwa teknolojia ya kidijitali na kwamba hata wajasiriamali na biashara zao hawana budi kwenda na wakati.

**WAKIRI UDHAIFU**

Mmoja wa wajasiriamali hao, Siasa Rajabu, anakiri kuwa kina mama wengi hawana elimu kuhusu TEHAMA, kitendo kinachosababisha washindwe kutangaza bidhaa zao na hata kuchangia kukwama kurejesha mikopo kwa wakati.

Anabaisha kuwa hawana soko ya uhakika, lakini anaamini kuwa kupitia elimu waliyopata watajitahidi kuwa wabunifu na kuboresha biashara zao ili wapate wateja wengi zaidi na kuomba uongozi wa Wilaya ya Bagamoyo kuvipa mikopo vikundi vya kinamama wajasiriamali.

# Ni pale baba alipogeuka mume kwa mama na binti

**INATOKA UK.11**

karatasi na kalamu ili kama anaogopa kumtaja aniandikie jina kwenye karatasi."

"Haikuwa rahisi kuamini aliandika ni baba halafu mbele jina kamili nikamwambia asome kwa sauti akasoma hivyo hivyo tena. Niliumia sana na nilipata shida sana kumweleza mdogo wangu hii aibu. Lakini hadi sasa hatujawaambia ndugu jambo gumu ambalo halijawahi kutokea katika familia yetu," anaeleza.

**KILIO CHA MAMA**

Mama mzazi Anelia Lyimo, anasema alipata taarifa za mtoto wake kusimamishwa masomo Februari 15 akiwa shambani huko Kimange karibu na Chalinze, baada ya kupigiwa simu kutoka shuleni kwake alimwomba dada yake aende kuupokea na kurudi na mtoto.

Anelia anasema alimpigia dada yake baada ya kuchukua mtoto huyo akae naye na kufanya mahojiano kuhusiana na mimba hiyo ili kumjua mhusika.

"Nilishangaa kuambiwa aliyempa mimba ni mume wangu niliumia na nililazimika kurejea usiku ule na kuwashirikisha polisi ambao siku iliyofuata alinipa vijana wa kwenda kumkamata mtuhumiwa akiwa shambani," anaeleza mama huyo.

Anasema baada ya kukamatwa mtuhumiwa alipelekwa kituo kidogo cha polisi Visiga na baadaye kuhamishiwa Mlandizi, akisubiri upelelezi kukamilika afikishwe mahakamani.

Kwa mujibu wa Anelea baada ya kupeleka baadhi ya nyaraka za mtoto zilizokuwa zikitakiwa polisi aliambiwa asubiri atapigiwa simu atakapohitajika.

**ANAPOKWAMIA**

"Kwasasa nimesimama kufuatilia kwasababu niliambiwa nilivyohitajika kuvipeleka vimekamilika nisubiri upelelezi ukamilike, kesi itapelekwa mahakamani na mimi nashindwa kufuatilia kutokana na kukosa nauli kila siku," anasema mzazi.

Mama huyo anasema kwa muda mrefu kumekuwa na kutoelewana kati yake na mumewe kutokana na tabia zake alizokuwa akionyesha.

"Kwanza alikuwa na tabia tukienda shamba anawahi kurudi nyumbani ananiacha peke yangu. Apanda pikipiki awahi nyumbani hakufikiria hata aliponiacha umbali mrefu. Hakuwa pia akinipatia matumizi nilikuwa na malalamiko mengi kwa ndugu zake na wasimamizi wetu wa ndoa," anaongeza Anilea.

"Ni kama nilikuwa nalea mwenyewe watoto wangu kwa maana fedha ya matumizi ilikuwa ngumu, lakini tabia yake ya kuwahi kurudi nyumbani na kuniacha shambani niliwatahadharisha watoto wangu wawe makini kwa kuwa hakuwa baba yao mzazi bali mlezi," anaeleza Anelia.

Anakumbuka kuwakanya watoto wake wa kike na wa kiume wasijenge ukaribu na baba yao huyo wa kambo kutokana na mienendo yake tangu afunge ndoa naye mwaka 2020.

"Kabla ya taarifa hizi za kumpa ujauzito mwanangu, amewahi kumsumbua binti yangu mkubwa nyakati za usiku, nikiwa shambani mbali na nyumbani, alipopiga kelele majirani wakatokea na wadogo zake huyu baba alitoka nje haraka na kujidai na yeye anashangaa," anasimulia mama huyo.

Aidha, anasema baada ya kukwama binti huyo aliendelea na visa ambavyo walikuwa wakifikishana kwa wasimamizi wao wa ndoa mara kwa mara na vingine kwa ndugu ambao hata hivyo hawakumpa ushirikiano wa kutafuta utatuzi.

"Kwa tukio hili la mwanangu ni kama huyu mwanaume amelipiza kisasi kwasababu mara nyingi amekuwa akinitafutia sababu kuwa huko shambani mbali nilipo kuna wanaume nakuwa nao na hata nikitafuta wafanyakazi kwa ujumla haniamini na hii inanipa sababu ya kuwa na hisia za kisasi," anasema.

Kadhalika, anasema anasubiri mpelelezi wa kesi hiyo ampigie simu kumweleza kinachoendelea, lakini anasema watu wengi wa hali ya chini wanakwama kufuatilia kesi kama hizo kutokana na kukosa fedha za mizunguko ya kwenda polisi mara kwa mara.

Mtendaji wa Kata ya Visiga, Aloysia Nyelo, amesema mara nyingi kesi za mimba hawapati mrejesho wake kwani baada ya kukabidhi polisi wakifuatilia wanaambiwa zinashughulikiwa katika dawati la jinsia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, amekiri kuwa na taarifa za mwanafunzi huyo kupata ujauzito na kwamba taratibu za mtuhumiwa kufikishwa mahakamani zinaendelea.

Lutumo anasema kesi kama hizo zikifika polisi zinashughulikiwa na kufikishwa mahakamani kwa hatua za kisheria.

ELIMU

NA JALIWASON JASSON, BABATI

# Fahamu sababu mwanao kumaliza shule pasipo kujua chochote, hata 'a'

ELIMU na lishe bora ni mapacha havitenganishwi, kwa vile mwanafunzi asipopata chakula asubuhi na mchana hawezi kuelewa masomo darasani. Kwa maelezo kuwa ubongo hautapokea anachofundishwa.

Ni ukweli huo unaowahamasisha wazazi, walezi na walimu kutetea upatikanaji wa chakula shuleni,

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Simon Mumbee, anasema.

Anaongeza kuwa chakula kina manufaa mengi, mosi kukua kimwili na kiakili kwa mwanafunzi, kuongezeka kimo na ubongo kufanyakazi.

Mumbee anasema wanafunzi wakikosa chakula bora hudumaa na hivyo wazazi wakichezea lishe kwenye umri wa miaka minne mpaka minane ambao wengi wao wanakuwa darasa la awali hadi la pili au la tatu wanaweza kusababisha ukuaji duni.

"Mtoto akikaa siku nzima bila kula anaathirika kiafya na uwezo wa kujifunza unaondoka,"anasema Mumbee.

Aidha, njaa huchangia utoro, ni chanzo cha kupiga miayo na usikivu hafifu darasani, anafafanua zaidi.

Kadhalika, kukiwapo na chakula mahudhurio huongezeka na wengi huipenda shule wakiwa na uhakika wa kula, anasema Ofisa Elimu na kwamba wanasimamia maelekezo ya waraka wa mwaka 2016 unaowataka wazazi au walezi kutoa chakula shuleni.

Mumbee anasema kwa mujibu wa waraka, wazazi na walezi wanatakiwa kubeba jukumu hilo na walimu kufundisha na ili kupata ufanisi, watendaji wa kata na walimu wamepewa maelekezo na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Babati na kwamba kila baada ya miezi mitatu kuna utaratibu wa kutathmini wanafunzi wangapi wanapata chakula shuleni na shule zote zinatoa chakula.

"Kila mzazi au mlezi anatakiwa kumchangia kilo 30 za mahindi kwa mhula, wanatakiwa kuzingatia hilo," anasema Ofisa Elimu Maalum Halmashauri ya Babati, Eveta Kavishe.

Anaongeza kuwa kati ya shule za msingi 148 za halmashauri hiyo, zinazotoa chakula cha mchana ni 142 na wamefanikiwa kwa sababu ya kulifanya suala hilo kuwa ajenda maalumu kwenye vikao vya Baraza la Madiwani.

Mwalimu wa awali kutoka Shule ya Msingi Maisaka wilayani humo, Raeikiel Mkanza, anasema madarasa ya awali yanapopata chakula kinaongeza furaha na ari ya kusoma na ufaulu, tena hakuna kusinzia darasani.



Wakili Ibrahim Mohamed, akiwaelezea wanafunzi wa Shule ya Msingi Olpopongi iliyoko Kiteto mkoani Manyara umuhimu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na ulazima wa chakula shuleni. **PICHA: JALIWASON JASSON**

"Wanaweza kutamka herufi kwa ufasaha hivyo nafasi ya chakula ni muhimu, akiongeza kuwa watoto wengi wa awali hawapati chakula usiku na asubuhi wanaamshwa kwenda shule wakiwa na njaa, akiwaasa wana familia kuwapa chakula asubuhi ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji.

Mwalimu Rehema Mwendo wa Kituo cha kulelea watoto cha kutwa cha Enhakore kilichoko Halmashauri ya Mji wa Babati anasema chakula shuleni ni muhimu tena chenye virutubisho vyote kwa kuwa watoto wanatakiwa wapate lishe bora.

Rehema anasema katika kituo chake anawapa uji saa nne asubuhi na chakula cha mchana saa 6:30 mchana na watoto anawapa matunda na mboga hivyo kila siku yanatolewa aina tofauti za matunda.

Anaeleza kuwa kula shuleni ni muhimu zaidi kwa kuwa chakula kinakuwa na usalama na tofauti na akirudi nyumbani anaweza asikute chakula maana wazazi wanakwenda kwenye shughuli zao.

ATHARI KUKIKOSA

Ofisa Elimu Mkoa wa Manyara, Halfani Masukira, anasema mwanafunzi anahudhuria shule siku 194 kwa mwaka, hivyo kila mlo mmoja kwa usiku, inamaanisha miaka saba ya msingi itakapomalizika anakuwa amekosa chakula miaka 3.6 mpaka anamalize shule.

"Ndiyo maana siku hizi wanafunzi wanamaliza masomo hawaeleweki ni kwa sababu wengi wao walikuwa wanashinda njaa hivyo akili zimedumaa.

Udumavu mwingine tunausababisha wenyewe wazazi na walezi, ukichangia chakula shuleni ni sawa amehamisha kutoka nyumbani kwenda shule ili mtoto ale mchana,"anasema Masukira

Januari Dalushi ni Ofisa Lishe wa Manyara anayenukuu utafiti wa mwaka 2015/2016, akisema ulibaini watoto wanapokelewa shuleni wakiwa na athari za kilishe.

Ananukuu utafiti kuwa asilimia 58 ya watoto chini ya miaka mitano walikuwa na upungufu wa damu na kwamba wa darasa la awali na la kwanza madhara wanayoweza kuyapata ni kinga kuwa chini hivyo ni rahisi kupata magonjwa kila mara na matokeo yake ni utoro.

Madhara mengine ni kukosa nguvu na uchovu wa mara kwa mara, kukosa usikivu darasani na vifo vinakuwa vingi katika umri huo.

"Tunaweza kuwadahili wanafunzi wengi wa darasa la awali na la kwanza ila tukawapoteza tusipowapa chakula," anasema Dalushi.

Mtaalamu huyo wa lishe anaeleza kuwa watoto hao umri huo ni wa msingi katika ukuaji ambapo anasema katika ukuaji wanaangalia awamu mbili ya kwanza ni miaka sifuri hadi miaka miwili na awamu ya pili ni kuanzia miaka mitano hadi miaka 18.

"Mtoto akishinda bila kula tumbo lake linakuwa wazi hivyo tunamwathiri ukuaji na usikivu darasani,"anaeleza.

Kiongozi huyo wa lishe anasema bado kuna desturi ya ulaji wa mazoea ila bado wanaratibu masuala ya chakula kwenye kamati za usimamizi za vijiji na Miata.

Anafafanua kuwa chakula kinachangwa ila wasimamizi ni lazima wahakikishe kina makundi matano ili kiwe bora, kiwe safi na virutubisho.

Mshauri wa awali wa malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC) Davis Gisuka, anasema ubongo ili uweze kukua kikamilifu ni lazima upate chakula bora ubongo, bila hivyo unadumaa.

Gisuka anasema kipindi kizuri cha kumwandaa mtoto ni kuanzia miaka 0 hadi nane na kwamba utafiti unaonyesha ukuaji wa ubongo na utendaji wa akili unakua kwa kasi mtoto akiwa na miaka mitatu mpaka minne ambapo ubongo unakua kwa asilimia 70 hadi asilimia 80 ya mtu mzima.

"Asipopata chakula mtoto atadumaa na hatasoma vizuri tutaishia kusema mtoto hana uwezo darasani kumbe alidumaa kwasababu ya kukosa chakula,"anasema Gisuka.

Analeza kushangazwa na wanafunzi wa darasa la awali kupewa chakula saa 5:00 asubuhi wakati wanataka kurudi nyumbani badala ya kupewa asubuhi saa 3:00 ili wawe makini darasani kumsikiliza mwalimu.

Gisuka anasema wanasisitiza siku 1,000 mama ale vizuri ili mtoto akizaliwa akue kikamilifu na katika kipindi hicho cha siku 1, 000 ndicho cha kumtengeneza binadamu bora.

Mtaalamu huyo anasema kuchangia chakula shuleni hakuna hasara ni sawa na kuhamisha chakula nyumbani na kupeleka shuleni, akiongeza kuwa kama tumbo halina chochote hata akili haina chochote pia.

Anafafanua kuwa chakula ndicho kinamjenga mtoto na kuna sababu za wazazi kuwekeza katika chakula maana wakipewa chakula kitafanikisha wanafunzi wa awali na darasa la kwanza kujua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Mratibu wa lishe shuleni kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Grace Shileringo, akizungumza kwenye kikao cha mapitio ya utekelezaji wa programu jumuishi ya taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM) anasema lishe shuleni ifuate muongozo wa lishe shuleni wa mwaka 2016 ili kuhamasisha wazazi na walezi kuchangia.

Anashauri mashamba ya shule yatumike kuzalisha chakula cha wanafunzi walime mboga, matunda na nafaka.

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM) ya 2021/22- 2025/26 lishe shuleni ni matokeo ya juhudi za wadau zinazotokana na ubunifu.

PJT-MMMAM inaeleza kuwa walimu au uongozi wa shule kuchangisha chakula kutoka kwa wazazi au walezi au ni kutokana na michango ya wasamaria wema.

Hata hivyo lishe hiyo haifikii kiwango bora cha vyakula mchanganyiko ambapo wadau kadhaa wanaohojiwa wanaonyesha kuwa uji wa nafaka pekee ndiyo unaotolewa.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Dk. Charles Msonde, akizungumza na wadau wa elimu mkoani Manyara mapema mwaka huu, anasema chakula shuleni siyo hiari ni lazima na kuhimiza utekelezaji.

ELIMU
**NA MWANDISHI WETU**

VITA VYA RUSSIA VS UKRAINE

# Ushindi wake uliko, ni zaidi ya teknolojia, silaha kali za kisasa

NI taifa lenye utaalamu, sayansi, teknolojia na mbinu za kila aina lakini linapopigana linachekwa kwa kushindwa. Kuna wakati liliingia vitani matunda machungu yakawa ni askari 58,000 kufa na kushindwa kijeshi katika vita vya Vietnam.

Lakini, leo limo kwenye vita vya Urusi na Ukraine nalo ni Marekani. Kwa mtazamo huo huenda sayansi na teknolojia wakati mwingine havileti ushindi badala yake huleta kuchekwa.

Vita vya Ukraine vinapopamba moto vinakumbana na mwangwi kuwa serikali ya Afghanistan iliyoundwa na Marekani pamoja na jeshi lake, vilianguka mwaka 2021 zikawa zama nyingine za Marekani yenye nguvu kubwa za kijeshi duniani, kurejea kilichotokea huko Vietnam.

Marekani ni mshirika namba moja wa Ukraine kwa kila kitu, silaha, mikakati, mifumo na mbinu za kisasa kuipiga Russia, lakini swali la kwa nini taifa hilo lenye nguvu zaidi duniani lilishindwa kujenga jeshi lenye uwezo wa Afghanistan hivi karibuni, leo litaisambaratisha Russia? Linaibuka.



Kifaru cha kisasa zaidi cha Marekani chenye teknolojia ya kielektroniki cha 'Abrams' kinachotegemewa kuwa mkombozi wa Ukraine vitani.

Mpango wa Marekani Afghanistan ulikuwa kujenga jeshi linaloweza kusimama kwa miguu yake kuwaangamiza waasi wa Taliban.

Mwishowe, hata hivyo, jeshi lilikosa ujasiri, lilishindwa kuundika na kufanya kazi ipasavyo kama lilivyoelekezwa na washauri elekezi wanajeshi wa Marekani.

Baada ya miaka 20 ya vita, Marekani inachomoka Afghanistan, ni sawa na ukweli kuwa uzoefu wake mbaya huko Vietnam Kusini, unajirudia tena, baada ya kushindwa kujenga jeshi la kisasa linakukomesha uasi na itikadi kali.

Lakini, kama nchi iliyoendelea kiviwanda, kisayansi, TEHAMA, elektroniki hadi kutua mwezini ukweli ni kwamba, taifa hilo kubwa halijawahi kushinda vita kikamilifu.

Ukiangalia kwa Ukraine, ukalinganisha na kile kilichotokea Afghanistan unaweza kusema, lengo lilikuwa kuunda vikosi vya usalama vya hali ya juu vinavyotumia teknolojia ya kisasa na mifumo ya vifaa vya kielektroniki, yote hayo hayakuwa ndani ya uwezo wa kile ambacho Afghanistan ingeweza kukitumia kwa njia endelevu.

Jambo zuri ni kuwa dunia na wengine wengi wamekuwa wakiliamini sana Jeshi la Marekani kwa miaka mingi kuwa lina nguvu ya teknolojia za kisasa ndege za droni zisizo na rubani, vifaru aina ya abrams na wataalamu kuanzia 'marine, wanamaji, anga, vikosi vya ardhini 'infantria' na majeshi ya ufukweni. Lakini mbona halishindi?

Hata huko Ukraine huenda lengo halitafikiwa mbali na Amerika kuuza vifaru vya kisasa, risasi, teknolojia na silaha za kila aina lakini kwa kurejea historia huenda hakutakuwa na ushindi.

**KUCHEKWA VITANI**

Kabla ya Afghanistan Amerika ilishiriki vita vya Iraq vilikuwa vya muda mrefu vikipiganwa kuanzia 2003 hadi 2011, uvamizi ukihusisha muungano wa majeshi unaoongozwa na Marekani, uliofanikisha kuipindua serikali ya Irak ya Saddam Hussein.

Hadithi ilianza kuwa Washington ilichochewa na mpango wa Sadam wa kumiliki silaha za maangamizi 'weapons of mass destruction'(WMD).

Silaha hizo kwa mujibu wa Marekani ni nyuklia, radiolojia, kemikali, wadudu zana za kibaiolojia au kifaa kingine ambacho kimekusudiwa kudhuru idadi kubwa ya watu na hilo lilitosha kuchochea vita.

**MWELEKEO WA WAMAREANI**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani wakati huo Condoleezza Rice anasema, "Hatutaki bunduki ya moshi iwe wingu la uyoga."

Licha ya Saddam kutokuwa na programu ya WMD, baadhi ya wataalamu wa Ushirikiano wa Kimataifa, wanaona kwamba awamu ya Rais George Bush, ilikosea kuanzisha vita.

Vita vya kwanza vilipigwa kuanzia Machi hadi Aprili 2003, vikosi vya Marekani na Uingereza na vya washirika kadhaa viliivamia Iraq na kuwashinda haraka wanajeshi wa Iraq na wanamgambo.

Ilifuatiwa na awamu ya pili vita virefu ambapo uvamizi wa Iraq unaoongozwa na Marekani ulipingwa na waasi. Baada ya ghasia kuanza kupungua mnamo 2007, Merekani polepole ilipunguza uwepo wa kijeshi nchini Iraqi na kujiondoa Desemba 2011, kwa mujibu wa Al Jazeera.

Mambo yalikuwa mabaya kwa upande wa Saddam Hussein alikamatwa, kushtakiwa na kuuawa, hivyo kuleta mabadiliko ya kiuongozi lakini suala la silaha za maangamizi likibakia kitendawili cha miaka mingi.

**VITA VYA LIBYA**

Marekani kwa kutumia jina la vikosi vya Muungano wa Umoja wa Kujihami (NATO), kama ilivyo kwa Urusi na Ukraine sasa, ilishambulia Libya kwa kutumia ndege zisizo na rubani, mizinga na kukabiliana na utawala wa Rais Muammar Qaddafi au Gaddafi, mwaka 2011.

Serikali ya Gaddafi ilidaiwa kufadhali operesheni za kigaidi dhidi ya Marekani, hasa shambulizi ukumbi wa disko huko Ujerumani kwenye 'Berlin discotheque mwaka 1986, na Amerika ililipiza kisasi kwa kuilipua Libya, na shambulio jingine lilikuwa la 1988 la ndege ya Marekani iliyotoka kwenye Uwanja wa Lockerbie nchini Scotland ikitarajiwa kutoa Amerika Uwanja wa John F Kennedy na kuua abiria wote 270 wakiwamo pia wafanyakazi.

Kisasi na dhamira ya kumwondoa Gaddafi ilikamilika Oktoba 2011 baada ya kunaswa, kukamatwa na kuuawa na majeshi ya ushirika kwenye mji wa Sirte na kuwa mwisho wa enzi ya kiongozi huyo.

Mzozo uliendelea hadi Oktoba 2019 lakini waasi wa Libya na wanamgambo wanaendelea na mzozo lakini majeshi ya Marekani yameondoka bila kushinda vita na kuiweka Libya kwenye mstari waliokuwa wanautaka.

**MOTO VIETNAM**

Vita vya Vietnam vilivyopiganwa katika ya miaka 1954 hadi 1975, ni mzozo wa muda mrefu katika historia ya Marekani ya kupinga Ukomunisti.

Ulihusisha Serikali ya Kikomunisti ya Vietnam Kaskazini na washirika wake huko Vietnam Kusini, inayojulikana kama Viet Cong, dhidi ya serikali ya Vietnam Kusini na mshirika wake mkuu, Marekani.

Ilijulikana kama "Vita vya Amerika" huko Vietnam na kiini cha mzozo huo kilikuwa na 'hamu' ya muungano ya Vietnam Kaskazini, ambayo ilishinda utawala wa kikoloni wa Ufaransa kwa Vietnam mnamo 1954.

Hamu ilikuwa ni kuunganisha nchi nzima chini ya serikali moja ya Kikomunisti iliyolengwa kuundwa kwa kuiga ile ya Umoja wa Kisovieti na China.

Serikali ya Vietnam Kusini, kwa upande mwingine, alipigana kuhifadhi Vietnam iliyokuwa karibu zaidi nchi za Magharibi hasa Marekani.

Ilipofika mwaka 1969 zaidi ya wanajeshi 500,000 wa Marekani waliwekwa nchini Vietnam. Wakati huo huo, Umoja wa Kisovieti na Uchina zilimimina silaha, vifaa, na washauri huko Vietnam Kaskazini. Nchi hizo zilitoa msaada, mwelekeo wa kisiasa, na wanajeshi wa wa kupigana kwa kampeni huko Kusini.

Gharama na hasara za vita vilivyokuwa vikiongezeka zilithibitika kuwa kubwa mno kwa Marekani kuzibeba, hivyo Marekani ilijiondoa, mwaka 1975 Vietnam Kusini ilikamatwa na kuwa sehemu ya Kaskazini chini ya Ukomonisti huku Jeshi lenye nguvu la Marekani likishindwa vibaya na kurudi nyumbani.

Pengine kitendawili au swali linaobaki; itakuwaje Moscow ni kama yaliyotokea Kabul waasi wanatawala hawajashindwa, au itakuwa kama Libya waasi wapo lakini Gaddafi ameondoka au kama Iraq Sadam hayupo lakini kote hakuna ushindi wa kujivunia?

***MITANDAO***





# Watendaji wapewa hadhari uporaji maeneo wananchi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MSTAHIKI Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, amewataka watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia uboreshaji na umiliki wa ardhi katika kata na mitaa kutojiingiza kwenye uporaji wa maeneo ya wananchi.

Aliyasema hayo juzi jijini hapo wakati akifungua mafunzo ya uboreshaji wa miliki ya ardhi kwa watendaji kata, madiwani, wenyeviti na wajumbe yaliyoandaliwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Alisema lengo la serikali kutambulisha mradi huo ni kuondoa kero za migogoro ya ardhi inayowakabili wananchi.

"Ninyi mliochaguliwa kuunda vikundi hivi kuanzia

madiwani, watendaji wa kata na mitaa pamoja na wajumbe wmliopendekezwa hakikisheni mnatenda haki kwa wananchi kwenye maeneo yao, msingeuke kuwa waporaji wa maeneo yao na mkifanya hivyo mtaondoa maana halisi ya serikali kupitia wizara husika ambayo imetoa fedha nyingi kwa ajili ya mradi wa uboreshaji na upimaji," alisisitiza.

Aidha, aliwataka watumishi hao kujikita kwenye kutoa elimu itakayowafanya kushiriki kwenye mradi huo ambao utaleta matunda ya kiuchumi.

Kadhalika, Prof. Mwamfupe alisema ili kufanikisha mradi huo kunahitaji ushirikiano kati ya wizara na watendaji husika kwani baadhi ya wananchi wamekuwa na hofu ya kuporwa maeneo yao ikiwamo viwanja, nyumba na mashamba.

Meneja Mradi Urasimishaji Mjini, Leons Mwenda, alisema mradi wa uboreshaji usalama wa miliki za ardhi unaotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa muda wa miaka mitano.

Alisema dhumuni la mradi huo ni kuongeza usalama wa miliki ya ardhi kwa kutoa hati miliki 2,000,000 pamoja na hati miliki za kimila 500,000.

Alisema mradi huo utajenga ofisi za ardhi katika mikoa 25 ili kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya utunzaji taarifa za ardhi pamoja na ukarabati wa ofisi katika halmashauri 41 nchini.

Aliongeza kuwa mradi huo utagharimu Sh.bilioni 345, ukiwa na lengo la kuimarisha miundombinu ambayo itarahisisha huduma za ardhi.

# Uhaba maofisa ugani chanzo sekta kilimo kutokuwa na tija

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

LICHA ya serikali kuweka nguvu kwenye sekta ya kilimo, imeelezwa kuwa uhaba wa maofisa ugani bado ni tatizo ambalo linachangia sekta hiyo kutokuwa na tija kwa wakulima.

Hivyo serikali imeshauriwa kuwekeza kwenye kilimo ekolojia ambacho kinalinda afya za watu na mazingira na kuachana na kilimo biashara ambacho kimekuwa kikihusisha matumizi makubwa ya kemikali.

Hayo yalibainisha juzi kwenye kongamano la huduma za ugani na kilimo ekolojia kwa wanawake, lililoandaliwa na Shirika la Action Aid na kujumuisha wakulima kutoka mikoa ya Singida, Morogoro, Dodoma na Songwe.

Janeth Nyamayahasi, mkulima kutoka Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, alisema kuwa uhaba wa maofisa ugani nchini umekuwa kikwazo kwao kushindwa kupata tija kwenye kilimo.

Alisema kutokana na uhaba wa maofisa ugani hasa katika maeneo ya vijijini wakulima wamekuwa wakilima kwa mazoea hali ambayo inawafanya washindwe kujikwamua kiuchumi kupitia sekta hiyo.

"Kwa mfano Wilaya ya Chamwino inavijiji 117 lakini maofisa ugani waliopo ni 50 na hawa wapo katika maeneo ya kata, hivyo mkulima hawezi kumsubiri ofisa ugani atoke kijiji kingine aje ampe mbinu za kilimo cha kisasa wakati msimu wa mvua unazidi kwenda,"alisema.

Alisema sera ya kilimo inasema kuwa ofisa ugani mmoja anapaswa kuhudumia kijiji kimoja na kuwafikia wakulima 600.

Alisema kero nyingine iliyopo kwenye sekta hiyo ni uhaba wa vitendea kazi ikiwamo vifaa vya kupimia afya udongo.

Naye Torati Buzika mkulima kutoka Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, alisema serikali inatakiwa kukipa kipaumbele kilimo ekolojia ambacho hakitumii kemikali.

Alisema kilimo ekolojia kwa kutumia mbegu za asili kinafaida nyingi ikiwamo kulinda afya za walaji pamoja na mazingira tofauti na mbegu za kisasa ambazo zinahitaji matumizi makubwa ya kemikali.

Ofisa Programu wa Action Aid, Elias Mtenda alisema lengo la kongamano hilo ni kuwakutanisha wakulima wanawake kutoka mikoa hiyo pamoja na wadau, wizara za kisekta na mashirika ili kuangalia kero za uhaba wa maofisa ugani na kutambua mbinu za kilimo ekolojia.




Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Devis Mwamfupe, akizungumza na madiwani, watendaji na wenyeviti wa mitaa na wajumbe wawakilishi wa wananchi kwenye mafunzo ya uboreshaji wa umiliki wa ardhi yaliyoandaliwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yaliyofanyika Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# OSHA yasajili maeneo 11,953 kwa miaka miwili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umesema kwa miaka miwili umefanikiwa kuongeza idadi ya maeneo ya kazi yaliyosajiliwa kutoka 4,336 hadi 11,953 ikiwa ni ongezeko la asimilia 276.

Mkurugenzi Mkuu OSHA, Khadija Mwenda, alibainisha hayo juzi wakati akitoa taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za wakala huo.

Adha, alisema idadi ya ukaguzi zilizofanyika zimeongezeka kutoka 104,203 hadi 322,241 sawa na ongezeko la asilimia 132. Alisema mafunzo hayo yanajumuisha usimamizi wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi na uundwaji wa kamati za usalama na afya, mafunzo ya kufanya kazi za mazingira ya juu.

Vile vile, alisema kuwa katika kipindi hicho kumekuwa na ongezeko la upimaji afya za wafanyakazi kwa asilimia 320.

"Upimaji afya kutoka wafanyakazi 363,820 hadi kufikia wafanyakazi 1,112,237 waliopimwa katika kipindi hicho," alisema.

Alisema ongozeko hilo lilitokana na kupunguza ada mbalimbali na kuboresha mifumo ya usimamizi ambayo imewezesha maeneo mengi ya kazi kukaguliwa, wafanyakazi wengi kupimwa afya na mafunzo mbalimbali kufanyika.

Mwenda alisema miongoni mwa majukumu ya OSHA ni kuchunguza ajali mbalimbali zinazotokea katika sehemu za kazi kwa lengo la kubaini vyanzo vya ajali hizo ili kushauri namna bora ya kuzuia kutokea tena.

Alisema kuwa katika kipindi cha miaka miwili ajali zilizoripotiwa zilipungua kwa asilimia 13.2 kutoka ajali 2,138 hadi 1,855.

Alisema magonjwa yanayotokana na kazi yalipungua kwa asilimia 22.1 kutoka wagonjwa 140 hadi 109.

Hata hivyo, alisema takwimu zinaonyesha kuimarika kwa mifumo ya usimamizi wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi, ambayo imepelekea ajali na magonjwa yatokanayo na kazi kupungua.





# 'Wazazi kutowahudumia watoto chanzo cha matukio ya ukatili'

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TABIA ya wazazi kujiegemeza zaidi kwenye shughuli za kiuchumi na kusahau majukumu ya kuwahudumia watoto ni chanzo cha kutokea matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ulawiti na ubakaji dhidi ya watoto.

Mwenyekiti wa vituo vya taarifa na maarifa vilivyoanzishwa na Mtandao wa Jinsia nchini TGNP, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Flora Mlowezi, alitoa kauli hiyo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Maadhimishi hayo yalifanyika katika Kata ya Ijombe Kijiji cha Nsongwi Matanji.

Alisema vitendo vya ukatili kwa sasa vimeshamiri kwa sababu wazazi hususani wanawake wamejikita zaidi kwenye shughuli za kutafuta pesa kuliko kuwahudumia watoto ambao wanahitaji ukaribu.

"Kinamama tupo bize sana kutafuta pesa kuliko kufuatilia mienendo ya watoto wetu, siyo shule wala nyumbani hatujui wana hali gani wanapitia mambo gani sisi ni pesa tu, tunasahau hizo fedha tunatafuta kwa ajili yao sasa wakibakwa au kulawitiwa tutakwenda kuzitafuta," alihoji Flora.

Akitoa mada katika maadhimisho hayo, Makamu Mwenyekiti wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, Oliver Kibona alisema wazazi wamewaachia jukumu ya kulea watoto walimu hali inayosababisha kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Aliwaasa wazazi kushirikiana na walimu kuwalea watoto ili kuwafundisha maadili mema na kuepukana na vitendo vinavyovunja maadili ya Mtanzania kama vile ushoga.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ijombe, Angumbwike Mwalesa, alisema baadhi ya wanawake wanavunja ndoa zao kwa sababu ya kukosa elimu ya kujitambua.

Alisema wanawake wanapaswa kuwa wanyenyekevu kwa waume zao licha ya baadhi yao kuwa na kipato kikubwa ili kuwalea watoto kwa pamoja.

Diwani wa Kata ya Ijombe, Marry Mbengele ambaye alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alisema kuwa wanawake wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kulinda haki za watoto.

Alisema Halmshauri ya Wilaya ya Mbeya, imetunga sheria mbalimbali kwa ajili ya ulinzi na usalama wa mtoto kwa kuzingatia miongozi ya sheria ya haki zao kupitia katiba na mikataba ya kimataifa.

"Tunawashukuru sana wadau wetu wakiwamo TGNP ambao wamekuwa karibu nasi kutujengea uwezo wa namna ya kupigania haki za watoto, wanawake na wenye ulemavu kwenye jamii yetu,"alisema Marry.

Aliongeza: "Elimu waliotupatia imetusaidia kupaza sauti na kuelimisha jamii kuachana na mila kandamizi ambazo zinachochea vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wenye ulemavu".

Kata nane za Mkoa wa Mbeya zilianzisha vituo vya taarifa na maarifa kwa kushirikiana na TGNP mwaka 2012 ambavyo lengo lake ni kutetea haki za wanawake, watoto na wenye ulemavu.

Matokeo ya kuanzishwa kwa vituo hivyo yameonekana ikiwamo upangaji wa bajeti zenye mlengo wa kijinsia katika halmashauri, uanzishwaji wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Galijembe iliyopo wilayani Mbeya pamoja na idadi kubwa ya wanawake kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.



Diwani wa Kata ya Ijombe wilayani Mbeya, Marry Mbengele, akitoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wanachama wa vituo vya taarifa na maarifa na wananchi dhidi ya wanawake, watoto na wenye ulemavu kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## M/kiti awataka madiwani kukusanya mapato kwa weledi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Bosco Mwanginde, amewataka madiwani wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanakusanya mapato kwenye maeneo yao.

Mwanginde alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kikao cha baraza la madiwani na kueleza kuwa ni muhimu suala la ukusanyaji mapato likatiliwa mkazo kwa sababu wilayani hiyo kwa sasa ina idadi kubwa ya watu kutokana na shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu na kilimo cha tumbaku.

"Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 Wilaya ya Chunya ina ongezeko la watu ukilinganisha na idadi ya watu kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 sasa kuna watu 344,471.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Chunya alikemea tabia za watoza ushuru ambao huwatoza wafanyabiashara na wakulima nje ya utaratibu akisema kuwa kwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria za nchi na ni kosa la uhujumu uchumi.

Alisema Jeshi la Polisi litawashughulikia mtoza ushuru yeyote atakayebainika kumtoza mwananchi fedha ambayo ipo kinyume na utaratibu.

Mayeka alitoa maagizo hayo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa madiwani kwamba kuna mawakala wa fedha wanamtaka mwananchi kutoa Sh.500.

**"Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 Wilaya ya Chunya ina ongezeko la watu ukilinganisha na idadi ya watu kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 sasa kuna watu 344,471.**

# Halmashauri yaua ngedere, mbwa wanaoharibu mazao

**Na Grace Mwakalinga,**
KYELA

UONGOZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya umewaua kwa kuwapiga risasi ngedere 33 na mbwa 79 baada ya wanyama hao kufanya uharibifu wa mali na mazao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira wa Halmashauri ya Kyela, Tumaini Mwakatika, alitoa taarifa hiyo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema walilazimika kuchukua hatua hiyo baada ya kupokea malalamiko kwa wananchi juu ya uharibifu uliofanywa na wanyama hao.

"Kumekuwa na idadi kubwa ya mbwa na ngedere ambao wanaharibu mazao ya wakulima na mali za wananchi tumepokea malalamiko mengi lakini tunawapongeza wananchi wetu hawakuchukua hatua za kuwajeruhi mpaka uongozi tulipokubaliana kuwaua," alisema Tumaini.

Tumaini aliomba wataalamu wa mifugo kutoa elimu kwa vijiji vyote kuhusu ufugaji holela wa mbwa bila kufuta utaratibu na kusababisha madhara huku akiwataka wananchi kufanya usafi kwa kupunguza miti ambayo imesababisha ngedere hao kujificha.

Aliongeza kuwa halmashauri hiyo ina uhaba wa wataalamu wa wanyamapori hali inayokwamisha juhudi za kupambana na wanyama hao kwani hakuna anayeweza kutumia risasi kuwaua wanyama hao.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, aliwasisitiza madiwani kusimamia ukusanyaji mapato ya halmashauri pamoja na kubuni vyanzo vipya sambamba na kutoa elimu juu ya mifumo ya ukusanyaji mapato ili wasipate vikwazo wakati wa ukusanyaji.

# SMZ yatoa ufafanuzi tetesi mfuko wa ZSSF kufilisika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) upo imara na unauwezo wa kulipa mafao wanachama wake kwa zaidi ya miaka 20 ijayo.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, wakati akitoa ufafanuzi na kujibu hoja za baadhi ya viongozi wa kisiasa waliodai kwamba ZSSF upo katika hali mbaya ya kufilisika kutokana na kutekeleza miradi ambayo haina tija.

Dk. Mkuya alisema siyo kweli kwamba ZSSF unatekeleza miradi ambayo haina tija inayoweza kusababisha mfuko huo kufilisika na kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kulipa mafao kwa wanachama wake.

Alisema mfuko wa hifadhi ya jamii unatekeleza miradi yenye tija ikiwamo ya ujenzi wa nyumba za makazi ambapo baadhi yake tayari zimeanza kutumika na kurudisha fedha katika kipindi kifupi.

Alisema katika muundo wa ZSSF ipo bodi ya uongozi ambayo ndiyo msimamizi mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake pamoja na mfuko kuwa na menejimenti yenye kusimamia shughuli za kila siku.

Alisema miradi yote kabla ya kutekelezwa kwanza inafanyiwa upembuzi yakinifu ikiwamo tathmini ya kina ikiwamo umuhimu wake na tija kwa mfuko pamoja na taifa kwa ujumla.

Aidha, alisema mfuko wa ZSSF unatarajia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023-2024 kuongeza mafao kwa wanachama wake wastaafu ikiwa ni dalili kwamba mfuko upo imara kifedha.

Alisema: "Mheshimiwa Naibu Spika niwaambie wananchi ikiwamo wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwamba upo imara ambapo unaweza kutekeleza majukumu yake ikiwamo kulipa fidia kwa wanachama kwa zaidi ya miaka 20 ijayo."

Hivyo, aliwataka wanasiasa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kufanya tathmini ya kina kabla ya kutoa taarifa kwa wananchi ambazo zinaweza kuzusha taharuki na wasiwasi mkubwa ikiwamo kwa wanachama wa mfuko huo.

# Daktari Bingwa: Wanaume wapenda ngono wanakufa mapema zaidi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

DAKTARI Bingwa wa Afya ya Uzazi kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Ummukulthum Omar, amesema wanaume wanaopenda kufanya ngono mara kwa mara wanakufa mapema ikilinganishwa na wengine.

Aliyasema hayo wakati akitoa mafunzo ya afya ya uzazi kwa wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar wakati wa mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika eneo la Tunguu Zanzibar.

Dk. Ummukulthum alisema wanaume wanaopenda kufanya ngono hufariki dunia mapema kwa sababu hutumia nguvu nyingi wanapofanya tendo hilo hali inayowasababisha kuishiwa nguvu mwilini.

Ingawa hakurejea utafiti mahususi wa kitabibu kuhusu hoja yake hiyo, Dk. Ummukulthum alisema kitaalamu mtu mmoja anatakiwa kufanya tendo la ndoa mara tatu kwa muda wa wiki moja ili kuufanya mwili kuwa imara.

"Kufanya tendo la ndoa kila siku kunahatarisha afya ya mwili, hivyo ni vyema wanandoa kufanya kitendo hicho kwa kufuata utaalamu kutoka kwa wataalamu wa afya na isiwe mnafanya jambo hilo kwa kukomoana,"alisema.

Akizungumzia kuhusu ukomo wa hedhi kwa wanawake, alisema kukoma kwa hedhi kwa mwanamke ni wastani wa miaka 45 hadi 55 kwa nchi za Afrika.

Alisema viashiria vya hedhi ni mabadiliko katika utokaji wake na kipindi hicho mwanamke anauwezo wa kupata mimba na kupata mtoto lakini hedhi inapofika ukomo mwanamke huwa hana uwezo tena wa kuzaa.

Alisema baada ya mabadikilo hayo, kipindi kinachofuata ni ukomo wa hedhi ambapo kitaalumu kinaitwa (Menopause) na hedhi huanza kukoma kwa muda wa miezi 12 mfululizo.

"Ili mwanamke ajijue kuwa hedhi yake imekoma ni kuhakikisha hapati hedhi kwa muda wa miezi 12 mfululizo,"alisema daktari huyo.

Alisema dalili zingine za kukoma kwa hedhi ni kupata maumivu wakati wa tendo la ndoa, kutokuwa na hamu ya tendo la ndoa, ukavu katika uke, msongo wa mawazo, kutokuwa na usingizi, kupata maradhi yasioambukiza na kuwa na joto kubwa mwilini.

Aidha, aliwataka wanawake kula vyakula vyenye afya bora hasa wakati wanapofika katika ukomo wa hadhi ili kuwa na afya njema mwilini.

Mwenyekiti wa Bodi ya TAMWA Zanzibar, Asha Abdi, alisema kuwa elimu ya afya ya uzazi inahitajika kwa wanawake hasa wasichana ambao wengi wao hujiingiza katika mapenzi wakiwa na umri mdogo bila ya kujua madhara yake.

Aidha, alisema elimu ya hedhi pia ni muhimu kwa wanawake kwa sababu wengi wao wanaokosa hedhi huwa na imani za kishirikina wakati wanakabiliwa na matatizo ya kiafya.



Daktari Bingwa wa Afya ya Uzazi, Ummulkurthumu Omar, akitoa mafunzo ya hedhi salama kwa wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar katika mkutano mkuu wa chama hicho ofisi za TAMWA Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yaitenga Mangapwani kuwa kituo kikuu cha biashara ya mafuta

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema eneo la Mangapwani kwa sasa litakuwa kituo kikuu cha biashara ya mafuta nchini.

Akizungumza kwenye hafla ya uzinduzi wa Bohari ya Mafuta Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi alizitaka wizara zinazohusika kuziambia kampuni za mafuta kuelekeza shughuli zote za mafuta kwenye eneo hilo.

"Serikali imekusudia kampuni zote za mafuta kushushia mafuta yao hapa Mangapwani," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema hatua za awali za ujenzi wa bandari hiyo ni kuanza kwa ujenzi wa barabara ya kilomita 60 ambayo itakuwa barabara ya kwanza kubwa na yenye ubora kwa Zanzibar na uwezo wa kuhudumia magari makubwa ya kubebea mizigo kulingana na uhalisia wa bandari yenyewe.

Dk. Mwinyi alisema Bandari ya Mangapwani itahusisha Bandari ya Makontena itakayokuwa na gati ya urefu wa kilomita moja itakayohudumia Ukanda wa Afrika Mashariki na makontena yatakayoshushwa bandarini hapo yataenda Dar es Salaam, Mombasa, Beira, Afrika Kusini.

Dk. Mwinyi alisema bandari nyingine inayotarajiwa kujengwa eneo hilo ni Bandari ya Nafaka itakayohusisha ushushaji wa bidhaa zote za vyakula ikiwamo mchele, maharage, mahindi, unga wa ngano na vyakula vingine.

Alisema ujenzi mwingine ni Bandari ya Mafuta itakayohifadhi lita milioni 21.

Dk. Mwinyi alisema bandari nyingine itakayojengwa kwenye eneo hilo ni Bandari ya Uvuvi itakayokidhi sera ya uchumi wa buluu.

Dk. Mwinyi alisema serikali inatarajia kuwa na mafuta ya kutosha na kuweka akiba ili Zanzibar iuze mafuta katika nchi mbalimbali zisizokuwa na bahari.

Alisema ujenzi wa Bandari Jumushi ya Mangapwani ni ufumbuzi wa changamoto zilizoko kwenye Bandari ya Malindi ambako meli hutumia siku tano hadi 10 kushusha mizigo hiyo, hali inayosababisha kupunguza uchumi wa nchi.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaib Hassan Kaduara, alisema wizara hiyo inagusa maisha ya watu ya kila siku na kueleza nia ya serikali yake kuwaondoshea wananchi matatizo yote yanayotokana na masuala ya maji, umeme na mafuta.

Alisema katika jitihada za serikali kupunguza kero hizo, inatarajia kuzindua tangi kubwa la majisafi na salama Chakechake Pemba, lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni moja ambalo litakuwa la kwanza kwa ukubwa Zanzibar.

Mkurugenzi wa masuala ya ushirika wa Kampuni ya Bakhresa, Hussein Sufiani, alishukuru serikali ya Zanzibar kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kutatua matatizo yanayowakabili wafanyabiashara.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**STEPHEN MAGRESSON KALANJE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **NS0794/0149/2010** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KINYALA SECONDARY SCHOOL mwaka 2010. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **DOD/DOD/RB/68131/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AHMED NDYAMUKAMA MTAJUKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya NISSAN X-TRAIL yenye usajili namba: **T334 CWN** na CHASSIS NAMBA: **NT30153783.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DSM/PHQ/RB/69918/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 103 YA 2022**

**KULWA DIONIZI LUSANA....................MLETA MAOMBI**

**DHIDI**

**NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC......,..........MJIBU MAOMBI**
**LJ.INTERNATIONAL LIMITED.............................MJIBU MAOMBI**
**MAJIGE SIMON MZULINGI..................................MJIBU MAOMBI**
**NATIONAL BANK OF COMMERCE LIMITED.................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA LJ.INTERNATIONAL LIMITED, MAJIGE SIMON MZULINGI**

Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 27/03/2023 mbele ya mwenyekiti E.Mogasa nyinyi wenyewe binafsi au mtume muwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 01 Mwezi Machi 2023.

E.Mogasa
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la Mdai 24, 2023**
**Jina la Mdai Robert Anselemi Luhega**
**Jina la Mdaiwa (1) Richard Leonard Mallya**
**(2)Linda Thomas Mkojera**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa: (1) Richard Leonard Mallya**
**(2)Linda Thomas Mkojera**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yao kwamba (eleza hapa habari za Madai )
Mdai ameleta madai dhidi yenu ya Tsh 1,950,000/=ambayo yametokana na fedha alizomkopesha bwana Richard L Mallya na alihaidi kulipa hajalipa na mdaiwa na 2 ulihaidi kulipa na hujalipa .Fika Mahakamani kujibu madai hiyo
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 14 mwezi 03 mwaka 2023 saa 06:00 Mchana kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28 mwezi 02 Mwaka 2023

.....................................................
**HAKIMU**
**Magistrate Court (Approved Forms for the Primary Court.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NGOMANILWA BALABIYU**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC. 919 CVP.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya polisi.
**KAH/RB/171/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**GODWIN JORAM NGOMANO,** Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne kilichotolewa na baraza la mtihani mwaka 2018 kupitia shule ya sekondari ya **MERRIWA SECONDARY SCHOOL**, chenye usajili wa namba CS 18049156 na Index namba **S. 126/0064**. kwa yeyote atakaefanikiwa kukiona atoe taarifa kituo chochote cha police au piga cm namba **0629528477. MOR/MOR/RB/80434/2023.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA DODOMA**
**LILILOPO DODOMA**

**RUFAA NA. 45 YA MWAKA 2022**

**CLEN MADIMILO......................................MRUFANI**

**VERSUS**

**RAULENSI URIO................................. MRUFANIWA**

**KWA: RAULENSI URIO**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayomaelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yoyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 27.03.2023 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibuwa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 27 ya Mwezi wa FEBRUARI,2023

.....................................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA
TANZANIA

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ANATY JUMANNE SIZYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yenye namba za usajili **MC 839CHS.**Chasis No. **LBRSPJB5XF011204.** Engine No. **15914029.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**GEI/GEI/RB/72887/2023.**


## PATA MKOPO KWA HARAKA

PATA MKOPO KWA HARAKA
**HADI 200,000,000/=**
KUTOKA
**ENTERPRISE FINANCE LIMITED**
KWAAJILI YA DHARURA
MBALIMBALI KAMA KULIPA
KODI YA NYUMBA,
KUNUNUA GARI,
KUBORESHA BIASHARA N.K

1173O3202

**TUNAPATIKANA**
DAR ES SALAAM **0677111333**
NA ARUSHA **0677226960.**


**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Amri ya **Mahakama ya Mwanzo Dodoma** Mjini nitauza **PAGALE Plot no. 59, Block ZM** MIGANGA Mkonze, mali ya SATIA SAMWELI SONGAMBELE ili kufidia deni analodaiwa mdaiwa katika shauri la Madai namba 240/2022 **(Alternative Microcredit Ltd dhidi ya Angelika Sendewa) Muda wa mnada ni saa 4:00 Asubuhi, tarehe 17/03/2023.**

**MASHARTI YA MNADA**

- Mnada utafanyika mahali Pagale lilipo/kiwanja kilipo
- Mnunuzi awe tayari kulipa 25% ya bei itakayofikiwa papo hapo na 75% atalipa ndani ya siku 14 baada ya siku ya mnada
- Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi

**KABLA YA SIKU YA MNADA**
**PIGA 0715 170 553**







TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Mtafaruku waibuka uchaguzi M/kiti TLP

**Na Halfani Chusi**

MTAFARUKU umeibuka kwenye Ofisi za Chama cha Tanzania Labour Party (TLP) baada ya Bodi ya Wadhamini kutangaza kuahirisha mkutano wa uchaguzi wa mwenyekiti mpya wa kumrithi aliyekuwa anayeshikilia kiti hiyo, hayati Augustino Mrema.

Mtafaruku huo uliibuka jana jijini Dar es Salaam, baada ya Katibu wa TLP Taifa, Richard Shedrack, kuwatangazia wajumbe waliofika kwenye mkutano kwamba uchaguzi hautakuwapo baada ya bodi kuona kuna viashiria vingi vya rushwa.

Kauli hiyo, iliwaibua wafuasi wa chama hicho na kuujia juu uongozi kupinga uamuzi huo wakitaka uchaguzi uendelee.

Katibu wa TLP mkoani Kilimanjaro, Esta Mlay, aliutaka uongozi huo, kuendelea na uchaguzi akidai ni aibu kwa chama hicho kukaa muda mrefu bila mwenyekiti.

"Nimekuja hapa kumchagua mwenyekiti, leo tunaambiwa mkutano umeahirishwa. Unadhani mimi nitawaeleza nini wanachama wangu loh! Hatukubali tunataka uchaguzi uendelee labda kama kuna kitu kimejificha, lakini mpaka jana wakati tunafanya kikao cha mwisho hakukuwa na shida iweje viongozi mhairishe?" Alihoji.

Huku akishangiliwa na wafuasi wa chama hicho wakiwamo wagombea waliokuwa wanaunga mkono hoja yake, alisema sio mara ya kwanza kwa chama hicho kuahirisha mkutano akidaia hata kipindi cha nyuma iliwahi kutokea.

Katibu wa TLP Dodoma, Damari Richard, alisema kuahirishwa kwa mkutano huo kunatia shaka, kwa sababu juzi walimaliza mkutano wao wa ndani kwa amani, lakini anashangaa kuambiwa uchaguzi umeahirishwa.

"Hilo linalozungumzwa habari ya vurugu sijui rushwa mimi sijaliona hakukuwa na shida hiyo, wanasingizia tu viongozi, mimi nilikuwa naomba uchaguzi uendelee apatikane mwenyekiti kila mtu arudi kwake akiwa anamjua kiongozi wake.

"Hiki ni chama kikubwa sana, na sisi ni wajumbe kutoka miaka mingi tupo kwenye chama hiki mambo kama haya yanatia aibu na tunapoteza imani kwa wafuasi wetu," alilalamika.

Mmoja wa wagombea wa nafasi ya uenyekiti, Stanley Ndamgoba, aliungana na wafuasi wa chama hicho kupinga kuahirishwa kwa uchaguzi huo akidai viongozi hawasemi ukweli.

"Leo wanatuambia uchaguzi umeahirishwa kwa sababu kulikuwa na ugomvi na viashiria vya rushwa hakuna ugomvi wala rushwa hapa, kama kuna viashiria hivyo kwa nini wasingeileta Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ije ichunguze?

Nipashe ilishuhudia wafuasi na wajumbe wa chama hicho, wakigomea kilichoamuliwa na viongozi wao wakidai wanataka uchaguzi ufanyike na sababu walizozitoa sio za kuvunja uchaguzi.

KATIBU AJIBU

Kutokana na malalamiko hayo, Katibu wa chama hicho, Richard Shedrack, aliwaeleza wafuasi hao sababu za kuahirishwa kwa mkutano huo ni pamoja na kuwapo kwa viashiria vya rushwa kwa viongozi wanaowania nafasi ya uongozi, kuzuka kwa vurugu kwenye mkutano wa halmashauri na ufinyu wa ukumbi kwa ajili ya kupigia kura.

Katibu Mwenezi wa TLP, Geofrey Steven, aliwaomba radhi wajumbe waliotoka mikoa mbalimbali kushiriki uchaguzi huo akiwataka kuwa watulivu kwenye kipindi hiki.

MSAJILI

Akizungumza na Nipashe, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Sisty Nyahoza, alisema ofisi yao haijatoa maelekezo yoyote kwa TLP na kama wakitoa kwa mujibu wa taratibu yanatakiwa yawe kwenye maandishi.

"Hayo ni mambo yao ya ndani, wenye mkutano ni wao, sisi ni waalikwa tu hatupangi kikao, mwalikwa hana nguvu ya kuahirisha mkutano bali walioandaa mkutano. Nasi tumepewa taarifa ya ghafla ya kuahirishwa kwa mkutano huu," alisema.

# Mlo chanzo cha tatizo la unene, ukondefu dar

**Na Mary Geofrey**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Rashid Mfaume, amesema licha ya mkoa huo kushika nafasi ya mwisho kwa tatizo la utapiamlo, watu wake wanakabiliwa na unene kupita kiasi na ukondefu.

Dk. Mfaume aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika hafla ya uzinduzi wa mfumo wa lishe kwa watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU) ulioandaliwa na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) kwa ushirikiano na Shirika la Chakula Duniani (WFP).

"Mkoa wa mwisho kwa udumavu ni Dar es Salaam, lakini inaonyesha tatizo ni huu unene na ukiangalia hapa wengi ni wanene wanene," alisema.

Pia alisema kumekuwapo upotoshaji wa kupata taarifa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu namna ya kupunguza mwili.

Alisema kuwapo kwa huduma hiyo ya mfumo (App) kutoka kwa TFNC itasaidia wakazi hao kupata taarifa sahihi za namna ya kupunguza uzito na unene kutoka kwa wataalamu.

"Unaingia kwenye mitandao kutafuta njia ya kupungua, mwingine anakuambia ufunge kwa saa 18 na wakati mwingine kuna App unaambiwa uingie ukifungua kumbe ni ya kulipia, ninaamini huduma hii mtaitoa bure ili wananchi wanufaike," alisema.

Dk. Mfaume aliongeza: "Wana Dar es Salaam tunafarijika sana kupata huduma hii, itatusaidia kupata taarifa za kupungua hasa kwa kuzingatia siyo watu wote wana uwezo sawa, kuna wanaojiweza sana, wenye uzito uliokithiri na kundi lingine linalotakiwa kuangaliwa sana."

Alitaja maeneo ya Temeke na Tandale, yana watoto wenye tatizo la kwashakoo, uzito pungufu na ukondefu.

Alishauri wataalamu hao kushirikiana na watoa huduma wa afya ngazi ya jamii, kutoa elimu ngazi ya kaya ili huduma hiyo kufikia wananchi wote.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alisema Tanzania imefanikiwa kupunguza udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano kutoka asilimia 34 mwaka 2015/16 hadi asilimia 30 mwaka huu.

"Bado serikali tuna kazi ya kufanya kufikia viwango vya kimataifa vinavyotaka tupungeze hadi kufikia chini ya asilimia 20. Kama serikali tunafanyia kazi afua mbalimbali za kuhakikisha tunapunguza tatizo hili nchini," alisema Prof. Nagu.

Aliwataka TFNC wawakutanishe wataalamu na wanasayansi kuhakikisha wanazifikia afua pamoja na kubadili programu mara kwa mara. Alisema nchini kuna tatizo la uzito uliozidi, viriba tumbo na takwimu za mwaka 2018 zinaonyesha kuwa, katika kila wanawake 10 walio na miaka 15 na 49, watatu wana tatizo la uzito uliozidi ambao ni sawa na asilimia 30.

Aliishauri TFNC kutumia app hiyo kutoa elimu ya mtindo bora wa maisha, mlo bora, kufikia wasichana walio katika umri wa kuzaa, wajawazito na wazazi njia salama za kutumia mlo kamili kupunguza matatizo mengi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFNC, Dk. Germana Leyna, alisema kwa kushirikiana na FAO, wameanzisha app hiyo inayolenga kusaidia kutoa elimu ya lishe kwa watu wanaoishi na VVU ili kupunguza athari zaidi.

Alisema mfumo huo utasaidia kuwapa taarifa sahihi za kuwasadia watu wanaoishi na VVU ili wafahamu vyakula wanavyotakiwa kula na baadaye wataandaa namna ya kupika vyakula.

"Lengo letu ni kumpa taarifa sahihi kwa wakati ili aweze kupata taarifa sahihi na kuondoa mila potofu kuhusu matumizi ya vyakula," alisema Dk. Germana.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza (kushoto), akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyofanyika kiwilaya, eneo la Bunju Dar es Salaam juzi na kuhudhuria na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, waliokaa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Anayedaiwa kuvunja kanisa asomewa mashtaka

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

ELPIDIUS Edward (26) amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mkoa wa Geita kwa makosa ya kuvunja Kanisa Kuu Jimbo Katoliki na kuharibu vitu mbalimbali vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni 48.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi, Nyakato Bigirwa na aliposomewa mashtaka yake alikana na kupelekwa mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Geita kwa kukosa wadhamini.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Winfrida Erenest, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Bigirwa alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Machi 20.

Hakimu huyo alimweleza mshtakiwa kesi yake ipo kwa Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Geita, Cloface Waane, yeye amemsomea hati ya mashtaka kwa sababu hakimu husika ana kazi zingine.

Akisoma hati ya mashtaka Wakili Winfrida, alidai kuwa Februari 26, mwaka huu katika mtaa wa Mbugani, Mkoa wa Geita mshtakiwa alivunja Kanisa Kuu Jimbo Katoliki la Geita na kuingia ndani kisha kuharibu vitu mbalimbali vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni 48, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

# BEKI WA MTIBWA SUGAR KUZIKWA LEO SHINYANGA

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Mtibwa Sugar, Idd Mobi Mfaume, aliyefariki Jumapili jioni katika Hospitali ya Benjamin Mpaka jijini Dodoma, anatarajiwa kuzikwa leo mjini Shinyanga.

Msemaji wa klabu hiyo, Tobias Kifaru, ambaye ni mmoja kati ya waliokuwa kwenye msafara huo tangu jana hospitalini hapo kwa ajili ya kukabidhiwa mwili wa marehemu, amesema kwa mujibu wa ndugu wa marehemu, mazishi yatafanyika leo saa saba mchana.

"Kwa upande wa Klabu ya Mtibwa Sugar, tumetekeleza kila kitu, ikiwamo usafiri pamoja na wajumbe wa kwenda kwenye mazishi ambao tumeambatana nao, nadhani kuanzia saa nne au tano (jana) tutakuwa tumeanza safari ya kuelekea Shinyanga na kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa ndugu wa marehemu, mazishi yatafanyika kesho saa saba pale Shinyanga, tumeshakabidhiwa mwili wa marehemu na kwa upande wa wachezaji wenzake yupo Mohamed Makaka na Vitalis Mayanga, watu wa benchi la ufundi pamoja na mimi mwenyewe," alisema Kifaru.

Kifaru alisema kifo cha beki huyo wa kati si pigo tu kwa Mtibwa Sugar, bali ni kwa familia yote ya michezo na taifa kwa ujumla kwani, mbali na kuzichezea klabu mbalimbali nchini, ameshawahi kuichezea Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Akizungumzia mazingira ya kifo chake, Kifaru alisema alianza kuumwa kichwa kuanzia Jumamosi jioni

"Alianza kuugua Jumamosi jioni majira saa 10 hivi, na aliposikia kichwa kinamuuma tulimwahisha hospitali ya kiwanda cha sukari Mtibwa kwa ajili ya uchunguzi, baada ya hapo tukiwa hospitali kubwa ya Misheni Turiani yenye wataalamu wazuri na vifaa, lakini ikaonekana bado, tukaamua kumpeleka Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma, tulifika huko majira ya saa saba usiku. Wakati wakifanya vipimo kuona nini kinasababisha ajisikie vibaya, jioni ya Jumapili mwenzetu akatutoka," alisema.

Mobi mwenye miaka 32, amewahi kuzichezea klabu mbalimbali za Ligi Kuu, zikiwamo Stand United, Polisi Morogoro, Polisi Tanzania, Mwadui FC na Ruvu Shooting, kabla ya kujiunga na Mtibwa Sugar.

PATASHIKA...



Vijana wa Timu ya New Boys, Johnson Ashiraf (kulia), akiwania mpira na mchezaji mwenzake, Franck Meshack, wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya nje vya Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Robo Fainali FA Cup timu za Ligi Kuu tu

**Na Adam Fungamwango**

MECHI za 16-bora za Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), maarufu FA Cup zinamalizika wiki hii huku timu zilizopo Ligi Kuu Tanzania Bara ndizo zilizotinga hatua ya robo fainali.

Timu zilizofanikiwa kutinga hatua hiyo ni Simba, Yanga, Azam, Ihefu FC, Mbeya City, Singida Big Stars, Geita Gold na Mtibwa Sugar.

Wakati wa kuelekea kwenye mechi hizo kulikuwa na timu tatu za madaraja ya chini ambazo ni African Sports, Pan African, Green Warriors na Mapinduzi FC ambazo zote zimetolewa, hivyo timu za madaraja ya chini kuishia kwenye hatua hiyo. Kati ya hizo, African Sports, Pan African na Green Warriors, zipo kwenye Ligi ya Championship ambayo bingwa wake na mshindi wa pili hupanda moja kwa moja Ligi Kuu na timu ya tatu na ya nne, hucheza mechi za mchujo kwa timu zinazoshika nafasi ya 14 na 13 kwenye Ligi Kuu. Mapinduzi FC ipo Ligi Daraja la Tatu.

Michuano hiyo ilianza Alhamisi kwenye Uwanja wa Uhuru, Simba ikiirarua African Sports mabao 4-0, yakifungwa na Jean Baleke, Kennedy Juma, Mohamed Mussa na Jimson Mwanuke.

Ijumaa, Yanga iliishindilia Prisons mabao 4-1, mawili ya Clement Mzize, Bakari Mwamnyeto na Aziz Ki, Jumna El Fadhili akiifungia Prisons bao la kufutia machozi na siku hiyo hiyo, Geita Gold ikiwa kwenye Uwanja wa Nyamkumbu, iliichapa Green Warriors mabao 3-1.

Ihefu iliichapa Pan African mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Highland Estates uliopo Mbarali, Mbeya, yote yakiwekwa wavuni na Andrew Simchimba ambaye ndiye kinara wa mabao kwenye michuano hiyo akifikisha saba, Mtibwa Sugar ikiilaza KMC bao 1-0 la David Kameta 'Duchu', mechi zikichezwa Jumamosi na juzi, Azam FC iliisulubu Mapinduzi FC mabao 2-0 yakifungwa na Cyprrian Kachewele na Nathaniel Chilambo, huku Mbeya City ikiidungua Kagera Sugar bao 1-0 kupitia kwa Richardson Ng'ondya.

## Mzize ataka namba aiue Real Bamako

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kung'ara kwenye mechi ya Kombe la FA hatua ya 16-bora akitupia mabao mawili katika ushindi wa 4-1 dhidi ya Tanzania Prisons, mshambuliaji kinda wa Yanga, Clement Mzize, amesema amejipanga vema kuivaa Real Bamako katika mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika endapo Kocha Nasreddine Nabi atampa nafasi ya kucheza hapo kesho.

Yanga itaikaribisha Real Bamako Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kesho, Jumatano ukiwa ni mchezo wa marudiano wa hatua ya makundi wa Kombe la Shirikisho Afrika baada ya timu hizo kutoka sare ya bao 1-1 wiki moja iliyopita nchini Mali.

Akizungumza na mwandishi wetu kuhusu mchezo huo, Mzize alisema atashirikiana na wachezaji wenzake kuhakikisha wanaipa ushindi timu yao ili iweze kusonga mbele katika mashindano ya kimataifa.

"Nimejipanga vizuri katika mchezo wetu ujao dhidi ya Real Bamako kwa kuendeleza ushindani wangu ili kuipa ushindi timu yetu," alisema Mzize.

## Kipanga yageukia kutetea Kombe FA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAAFANDE wa timu ya Kipanga, wamesema mkakati wao kwa sasa ni kutetea Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, baada ya kuukosa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

Timu ya Kipanga ambao ndio mabingwa watetezi wa Kombe hilo wamesema juhudi na nguvu zao zote wanazihamishia katika michuano hiyo ili kutimiza lengo lao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Swalehe Maalim, alisema licha ya kuendelea na maandalizi ya michezo ya Ligi Kuu Zanzibar ambayo wanahaha kujinasua kushuka daraja, bado wanaendelea na kampeni yao ya kutetea ubingwa wa FA.

Alisema uongozi wa timu hiyo unatarajia kuwahamasisha wachezaji ili kuhakikisha wanatimiza lengo lao la kutetea Kombe la FA ikiwamo kutoa hamasa hata ya zawaidi iwapo watafanikiwa.

"Kwa upande wetu viongozi, tumejipanga zaidi kuhakikisha tunawahamasisha wachezaji ili kuvumilia hatua hii ya 36 na hatimaye kunyakuwa ubingwa, matumaini yetu hamasa hii itafanikiwa endapo wachezaji watajituma," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**BRUNO AWANIWA MADRID**
REAL Madrid pia inawania kumsajili kiungo wa Newcastle United mwenye umri wa miaka 25, Bruno Guimaraes. ***(Mundo Deportivo)***

**MOUNT AWINDWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL wataongoza mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Chelsea na England, Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24 wakati wa kipindi cha majira ya joto, baada ya kukataa kukubali kusaini mkataba mpya pale Stamford Bridge. ***(Mail)***

**GVARDIOL ATAKIWA CHELSEA**
CHELSEA imefufua nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa RB Leipzig, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 21, huku Manchester City na Tottenham Hotspur zikimwania mchezaji huyo wa Kimataifa wa Croatia ambaye ana kipengele cha kuondoka kwa pauni milioni 97. ***(Times)***

**KEITA KUTUA MILAN**
INTER Milan ina matumaini ya kumsajili, Naby Keita, mwenye umri wa miaka 28 wakati mkataba wake utakapomalizika pale Liverpool. ***(Gazzetta dello Sport)***

**ROMEO ATAKIWA UNITED**
KLABU ya Manchester United imejiunga na Chelsea na Arsenal kwenye mbio za kumwania kiungo wa Southampton mwenye umri wa miaka 19, Romeo Lavia raia wa Ubelgiji. ***(Mail)***

**SPURS YAMTAKA SCOTT**
KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumsajili kiungo wa Bristol City, Alex Scott. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 19, raia wa England pia anawaniwa na Crystal Palace na West Ham. ***(Sun)***

**FERGUSON NA LEICESTER**
LEICESTER City na Everton zinamfuatilia kiungo wa Bologna na Scotland, Lewis Ferguson, mwenye umri wa miaka 23. ***(Nicolo Schira)***

**SOLOMON AWINDWA FULHAM**
KLABU ya Fulham wanataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu winga wa Israel mwenye umri wa miaka 23, Manor Solomon kutoka Shakhtar Donetsk ambaye yupo hapo kwa mkopo. ***(Standard)***

**BRUNO MKATABA MPYA**
KLABU ya Newcastle United ina uhakika wa kukubaliana mkataba mpya ambao utamweka kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes, mwenye umri wa miaka 25, katika klabu hiyo kwa muda mrefu. ***(Football Insider)***

**MADDISON ATAJWA NEWCASTLE**
KIUNGO wa kati wa Leicester City na England, James Maddison, mwenye umri wa miaka 26, yuko kwenye orodha fupi ya wachezaji wanaolengwa na Newcastle United majira ya joto, pamoja na kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay. ***(Football Insider)***

**MBAPPE ANA FURAHA**
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 24, amesema “ana furaha sana” katika klabu hiyo na mustakabali wake hauhusiani na maendeleo ya mabingwa hao wa Ufaransa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(90min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG ATAKA MAELEZO YA WACHEZAJI KIPIGO LIVER

Kuna mambo mengi yananikera, lakini kuruhusu mabao kwa urahisi hivyo bila shaka ni mojawapo...

**LIVERPOOL, England**

ERIK ten Hag amesema atawakusanya wachezaji wa Manchester United na kuwapa nafasi ya kueleza uchezaji wao mbaya uliosababisha kufungwa mabao 7-0 na Liverpool kwenye Uwanja wa Anfield, Jumapili.

Baada ya kipigo kikali zaidi katika maisha ya kocha huyo wa Uholanzi kwenye michezo 481, Ten Hag alipendekeza kuwapo mazungumzo ya mara moja kwenye chumba cha kubadilishia nguo kwamba yalikuwa ndio njia kuu.

‘Mashetani Wekundu’ hao wameruhusu mabao 21 katika mechi tano za ligi dhidi ya Liverpool, na hawajawahi kupoteza mechi ya ushindani kwa tofauti ya mabao zaidi ya saba.

Ten Hag alisema: “Kama timu, mnatakiwa kushikamana na hilo ndilo ambalo hatukufanya. Ilikuwa ni mshangao kwangu. Sijaona hili kutoka kwa timu yangu na sidhani kama ni sisi. Sidhani kama ni Manchester United. Kwa hivyo ni mbaya na mbaya sana.”

Ten Hag alipoulizwa iwapo wachezaji walitoa maelezo ya mchezo huo wa kipindi cha pili, alisema: “Sikuwapa nafasi hadi sasa. Nimetoa maoni yangu kuhusu hilo, tutalizungumza kesho. Lakini najua, timu hii itawekwa upya na inabidi turudi nyuma.

“Kuna mambo mengi ambayo yananikera, lakini kuruhusu mabao kwa urahisi hivyo bila shaka ni mojawapo.”

“Nimekuwa na siku mbaya, lakini siku zingine ikiwa utafanya mambo sahihi, ikiwa unachukua hatua sahihi kama kocha na kama timu, basi unaweza kujifunza mengi.

“Kama ilikuwa mara nyingi zaidi bila shaka basi ni muundo, lakini tulikuwa na matokeo mengi mazuri katika wiki zilizopita.

“Huu ulikuwa uchezaji mbaya sana na ninazungumzia kipindi cha pili, kwa sababu katika kipindi cha kwanza timu ilicheza vizuri sana.”

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,087,3

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 07 NA 08 MACHI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/03/23 | 22:45 | Huddersfield vs Bristol City | 2.54 | 3.14 | 2.64 |
| 02. 07/03/23 | 22:45 | Walsall vs Bradford City | 2.54 | 2.88 | 2.78 |
| 03. 07/03/23 | 22:45 | Cheltenham vs Lincoln | 2.48 | 3.20 | 2.65 |
| 04. 07/03/23 | 23:00 | Plymouth vs Derby | 2.70 | 3.25 | 2.42 |
| 05. 08/03/23 | 01:00 | Audax Italiano vs Universidad Catolica | 2.95 | 3.01 | 2.33 |
| 06. 08/03/23 | 01:00 | Tacuary Asuncion vs Club General Caballero Jlm | 2.47 | 3.37 | 2.52 |
| 07. 08/03/23 | 13:00 | Shonan Bellmare vs Urawa Red Diamonds | 2.40 | 3.05 | 2.55 |
| 08. 08/03/23 | 13:00 | Vissel Kobe vs Nagoya Grampus | 2.22 | 3.15 | 3.00 |
| 09. 08/03/23 | 13:00 | Sagan Tosu vs Consadole Sapporo | 2.51 | 3.27 | 2.53 |
| 10. 08/03/23 | 13:00 | Kyoto Sanga vs Gamba Osaka | 2.29 | 3.20 | 2.84 |
| 11. 08/03/23 | 13:00 | Kashiwa Reysol vs Kashima Antlers | 2.75 | 3.32 | 2.30 |
| 12. 08/03/23 | 16:30 | Liptovsky Mikulas vs MFK Skalica | 2.55 | 3.15 | 2.55 |
| 13. 08/03/23 | 18:00 | Ismaily SC vs Farco FC | 2.50 | 2.71 | 3.16 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · halopesa · airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA AMSHUKIA DE BRUYNE KIWANGO



**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anataka Kevin De Bruyne arejee kwenye misingi yake ili kurudi katika kiwango chake bora.

Mchezaji huyo bora wa msimu uliopita Ligi Kuu England, alikosa michezo miwili kutokana na kuwa majeruhi.

Mbelgiji huyo hakuwa na kiwango kizuri dhidi ya Newcastle United katika ushindi wa mabao 2-0 siku ya Jumamosi na alibadilishwa na Bernardo Silva.

De Bruyne alipata matokeo mazuri baada ya kufunga bao zuri katika ushindi wa mabao 3-0 wa City wa Kombe la FA dhidi ya Bristol City wiki iliyopita, lakini Guardiola alisema hakuwa kwenye ubora wake.

"Kila mtu anakijua kiwango chake, ndani ya wiki moja ana nafasi ya kuonyesha ubora wake, amefurahishwa na ushindi tulioupata, hiki ndicho tunachotakiwa kufanya. Turudi kwenye kanuni, tufanye kazi kwa bidii."

De Bruyne amefunga mabao manne na kutoa asisti 12 kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku City wakishika nafasi ya pili, pointi tano nyuma ya Arsenal.

City wana mapumziko ya katikati ya juma bila kucheza mechi yoyote na kuwaruhusu wachezaji kupumzika na kupata nafuu kabla ya safari ya Jumamosi ya ligi dhidi ya Crystal Palace na kisha kuwakaribisha RB Leipzig katika mechi ya marudiano ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Guardiola alisisitiza umuhimu wa mechi zote mbili kwa msimu wao.

"Tunajiandaa vema kwa ajili ya mchezo dhidi ya Crystal Palace, kila mara ilikuwa ngumu kwetu," alisema Guardiola.

# Ancelotti hataki kukata tamaa LaLiga

**MADRID, Hispani**

CARLO Ancelotti ameapa Real Madrid hatakata tamaa kuiwinda Barcelona kileleni mwa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, licha ya timu yake kuachwa kwa pointi tisa.

Madrid walilazimishwa sare tasa na Real Betis katika siku ambayo ingeweza kuwa muhimu kwenye mbio za ubingwa, saa chache baada ya wachezaji 10 wa Barcelona kushinda nyumbani kwa bao 1-0 dhidi ya Valencia.

Baada ya kuona kikosi chake kikishikiliwa kwa mchezo wa pili wa ligi, kutokana na kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Atletico Madrid wiki iliyopita, Ancelotti alikubali Madrid wana kazi kubwa.

"Si jambo lisilowezekana," alisema akiiambia Movistar wakati alipoulizwa kama kuna matumaini yoyote ya kuinasa Barca.

"Itakuwa ngumu sana, ngumu sana, lakini hatuna shaka tutapambana hadi mwisho.

"Bila shaka matokeo haya yanaathiri timu. Ikiwa haifanyi hivyo basi huna nafasi ya kuimarika."

Madrid hawajashinda katika mechi tatu baada ya kufungwa 1-0 na Barcelona katika mechi ya kwanza ya nusu fainali ya Copa del Rey Alhamisi.

Mabingwa hao wa Ulaya wameshindwa kufunga katika michezo yao miwili iliyopita.



HABARI MICHEZO

305,640/-

# SIMCHIMBA AMSHUSHA MZIZE UFUNGAJI BORA KOMBE LA FA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuongoza kwa ufungaji kwenye michuano ya Kombe la FA kwa saa zisizozidi 24, straika wa Yanga, Clement Mzize, alienguliwa kwenye nafasi hiyo Jumamosi na aliyekuwa akiongoza awali, Andrew Simchimba wa Ihefu FC, ambaye amerejea kwenye nafasi yake.

Simchimba alifunga mabao yote mawili Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya, akiipa ushindi timu yake ya Ihefu wa mabao 2-0 dhidi ya Pan African ya Dar es Salaam na kumfanya kufikisha mabao saba.

Awali, straika huyo alikuwa kinara wa mabao kwenye michuano hiyo, akipachika matano nyavuni hadi kuingia kwenye hatua ya 16 bora, lakini Ijumaa iliyopita alienguliwa na Mzize, aliyefunga mabao mawili kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, akiiongoza Yanga kupata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Tanzania Prisons.

Mabao hayo ya straika huyo chipukizi wa Yanga aliyekuwa tayari amecheka na nyavu mara nne hapo awali, yalimfanya kufikisha sita, akimwengua Simchimba aliyebaki na mabao yake matano.

Hata hivyo, Mzize hakudumu kileleni, kwani Jumamosi Simchimba alirudi kwenye kiti chake cha uongozi, akipachika mabao mawili, dakika ya 23 kwa mkwaju wa penalti, baada ya Yacouba Songne kuangushwa kwenye eneo la hatari, lingine akilipachika dakika ya 47, akiwa amefikisha mabao saba.

Ushindi huo umeifanya Ihefu kuungana na Simba, Yanga, Singida Big Stars na Mtibwa Sugar kwenda hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ambayo bingwa wake anaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Mtibwa ilipata nafasi hiyo juzi, ilipoifunga KMC bao 1-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, shukrani kwa David Kameta 'Duchu' aliyezamisha mpira kimyani na kuipa timu yake ushindi.

Wachezaji wenye mabao manne mpaka sasa kwenye michuano hiyo ni Moses Phiri wa Simba, Richardson Ng'ondya wa Mbeya City na Sadala Lipangile wa KMC.

## Simba: Ni ushindi tu leo

INATOKA UK. 24

katika mchezo huo kwa kuvuka katika hatua ya makundi na kucheza robo fainali.

"Ni mechi ngumu na ushindani mkubwa, mipango yetu dhidi ya Vipers ni kushinda katika mchezo huo, mpira ni sasa si muda uliopita au utakaokuja kwa Simba tunaangalia kilichopo mbele yetu.

"Mbele yetu ni mechi ya Vipers kwa kushinda mchezo wa leo, huwezi kucheza mechi vizuri kwa muda wote, tunajiandaa vizuri kulingana na mpinzani wetu," alisema Robertinho.

Mwakilishi wa wachezaji wa Simba, Shomari Kapombe, alisema wachezaji wako vizuri na wanajua umuhimu wa mchezo huo ni kutafuta ushindi tu.

Alisema wamerudi uwanja wa nyumbani kwa mawazo tofauti ya mechi iliyopita ambayo walipoteza nyumbani dhidi ya Raja Casablamnca na sasa hawataki kurejea makosa yaliyopita na hakuna wanachokitaka zaidi ya ushindi dhidi ya Vipers.

"Tumejiandaa kurudisha ile hali ya awali ya anayekanyanga katika uwanja wa nyumbani, kwa sababu tunahitaji ushindi katika mchezo huu, kutafuta pointi tatu na kucheza kwa tahadhari kubwa na aina ya wapinzani wetu," alisema Kapombe.

Kocha Mkuu wa Vipers, Roberto Bianch, alisema anafuraha kuja tena Tanzania, na amerudi kwa ajili ya kuchukua pointi tatu zitakazowafanya wafuzu hatua inayofuata kwani kimahesabu wana nafasi hiyo.

"Tulicheza vizuri dhidi ya Simba, tukatengeneza nafasi nyingi tukashindwa kuzitumia, tulipoteza kutokana na uzoefu wa wachezaji wa Simba kwenye mipira ya kutenga.

"Kwenye michuano ya CAF unaadhibiwa kutokana na makosa yako tumejipanga kuhakikisha haturudii tulichofanya kwenye mchezo uliopita, kuna mabadiliko kadhaa tunaenda kuyafanya ikiwamo baadhi ya wachezaji," alisema Bianchi.

## Fei Toto, Yanga

INATOKA UK. 24

TFF kumshtaki Fei Toto kwa madai ya kuandika barua ya kuvunja mkataba isivyo halali, ambapo kamati iliamua kuwa mchezaji huyo ni mali ya klabu hiyo, lakini mwenyewe alipinga na kutaka marejeo ya kesi hiyo, ambapo pia alibwagwa akiambiwa uamuzi wa awali unabaki kama ulivyo. Kwa muda mrefu sasa, tangu mwishoni mwa mwaka jana, Feisal amekuwa hana maelewano mazuri na klabu yake, ambapo kuna wakati alilazimisha kuondoka kwa kutumbukiza kiasi cha pesa kwenye akaunti, lakini klabu ilizirejesha, huku mwenyewe akiwa ameshaandika barua ya kuaga akiwashukuru Wanayanga wote, viongozi, wachezaji, wanachama na mashabiki.

Kwa utaratibu huo wa kuwasilisha barua TFF ya kutaka kuvunja mkataba na Yanga, ni wazi sasa ametambua bado ana mkataba hai na klabu hiyo ili hilo litekelezeke pande mbili lazima zikae meza moja ya mazungumzo na kukubaliana.

Wakati huo huo, winga mtukutu raia wa Ghana, Bernard Morrison, ameanza mazoezi na kikosi chake cha Yanga, tayari kukitumikia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Ligi Kuu na Kombe la FA, baada ya kukaa nje akiuguza majeraha ya nyonga.

Akizungumzia matayarisho ya mechi ya kesho dhidi ya Real Bamako ya Mali, utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe amesema moja ya habari njema ni urejeo wa Morrison ambaye amekosekana kwa muda mrefu na sasa ameanza mazoezi ya pamoja na wachezaji wengine.

"Tumepata habari njema, ni kwamba mchezaji wetu Morrison ameanza mazoezi ya uwanjani kwa maana alikuwa nje kwa muda mrefu, alikuwa anauguza majeraha yake ya nyonga, lakini kwa sasa ameanza mazoezi pamoja na timu," alisema Kamwe.

Hata hivyo alisema mchezaji huyo hatoweza kuwamo kwenye kikosi kitakachoivaa Real Bamako, lakini kama mambo yatakwenda vema na kurejesha utimamu wa mwili haraka, atakuwapo kwenye kikosi kitakachoivaa US Monastir ya Tunisia utakaochezwa Machi 19, mwaka huu nchini, kwa sababu lengo kubwa lao ni kuongoza kundi.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/03/23 | 18:00 | Everton FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 02. 11/03/23 | 18:00 | Preston North End vs Cardiff City | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 03. 11/03/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Watford FC | 2.65 | 3.15 | 2.50 |
| 04. 11/03/23 | 18:15 | Elche CF vs Real Valladolid | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 05. 11/03/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs Santa Clara Azores | 2.31 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 11/03/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KV Oostende | 2.46 | 3.30 | 2.60 |
| 07. 11/03/23 | 22:45 | Bologna FC vs Lazio Rome | 2.95 | 3.15 | 2.29 |
| 08. 11/03/23 | 23:00 | Sparta Rotterdam vs Vitesse Arnhem | 2.35 | 3.25 | 2.80 |
| 09. 12/03/23 | 14:15 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.45 | 3.20 | 2.70 |
| 10 12/03/23 | 14:30 | US Lecce vs Torino FC | 2.85 | 2.90 | 2.55 |
| 11. 12/03/23 | 16:00 | RCD Mallorca vs Real Sociedad San Sebastian | 3.20 | 2.85 | 2.36 |
| 12. 12/03/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs Montpellier HSC | 2.75 | 3.10 | 2.50 |
| 13. 12/03/23 | 17:00 | FC Nantes vs OGC Nice | 3.05 | 3.10 | 2.28 |
| 14. 12/03/23 | 17:00 | Hellas Verona vs AC Monza | 2.36 | 3.05 | 2.95 |
| 15. 12/03/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs Gil Vicente Barcelos | 2.28 | 3.10 | 3.05 |
| 16. 12/03/23 | 20:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.29 | 3.40 | 3.05 |
| 17. 12/03/23 | 21:30 | VfL Wolfsburg vs Union Berlin | 2.26 | 3.20 | 3.30 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 07/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5670 | Bali Utd Pusam vs Persita Tangerang | 1.56 | 3.70 | 4.40 |
| 15:50 | 5756 | AL Qaisoma vs Al Faisaly (KSA) | 4.74 | 3.14 | 1.72 |
| 16:00 | 2416 | AL Khlood vs Alshoulla | 1.82 | 3.04 | 4.32 |
| 16:00 | 4464 | Sidama Bunna SC vs Dire Dawa Kenema FC | 2.06 | 2.95 | 3.15 |
| 16:30 | 5841 | Tatran Presov vs AS Trencin | 3.36 | 3.31 | 2.00 |
| 17:00 | 3017 | Pendikspor vs Tuzlaspor | 1.56 | 3.75 | 4.93 |
| 17:00 | 4454 | CS Constantine vs JS Kabylie | 1.85 | 2.99 | 4.44 |
| 18:00 | 5840 | Al Ahly Cairo vs Arab Contractors | 1.45 | 4.04 | 6.87 |
| 18:30 | 2490 | Al Hidd Club vs AL Khalidiyah | 5.40 | 3.50 | 1.50 |
| 18:30 | 4868 | Riffa Club vs Al Ahli Manama | 1.54 | 3.45 | 5.00 |
| 18:45 | 3609 | Najran SC vs Al Ahli Jeddah | 6.34 | 3.79 | 1.45 |
| 19:00 | 1417 | Aris Limassol vs Anorthosis Famagusta | 1.82 | 3.59 | 3.95 |
| 19:00 | 1623 | Saint George FC vs Ethiopian Medhin | 1.47 | 3.70 | 5.40 |
| 20:00 | 3522 | Olympiakos Nicosia vs Pafos FC | 5.28 | 3.91 | 1.57 |
| 20:00 | 4423 | Altinordu vs Goeztepe | 2.67 | 3.13 | 2.40 |
| 20:00 | 4712 | Gloria Buzau vs Unirea Slobozia | 2.12 | 3.13 | 3.13 |
| 20:30 | 4101 | Backa Topola vs Red Star Belgrade | 5.74 | 4.10 | 1.45 |
| 20:45 | 3680 | Lazio vs AZ Alkmaar | 1.66 | 3.84 | 4.64 |
| 22:45 | 1021 | Dagenham and Redbridge vs Wrexham | 4.83 | 3.99 | 1.59 |
| 22:45 | 1308 | Maidenhead U vs Boreham Wood | 2.95 | 3.22 | 2.30 |
| 22:45 | 1357 | Bromley vs York City | 1.99 | 3.35 | 3.51 |
| 22:45 | 1386 | Peterborough vs Shrewsbury | 1.74 | 3.57 | 4.43 |
| 22:45 | 1529 | Barnsley vs Portsmouth | 2.03 | 3.28 | 3.54 |
| 22:45 | 1697 | Sutton United vs Crawley Town | 1.62 | 3.61 | 4.85 |
| 22:45 | 1721 | Larne vs Linfield Belfast | 2.29 | 2.97 | 2.97 |
| 22:45 | 2046 | Grimsby vs Newport | 2.28 | 3.18 | 2.88 |
| 22:45 | 2285 | Southend vs Chesterfield | 2.50 | 3.21 | 2.68 |
| 22:45 | 2700 | Dorking Wanderers vs Barnet | 3.14 | 3.67 | 2.02 |
| 22:45 | 2806 | Huddersfield vs Bristol City | 2.79 | 3.14 | 2.42 |
| 22:45 | 3112 | Ipswich vs Accrington | 1.25 | 5.46 | 10.11 |
| 22:45 | 3140 | Gateshead vs Halifax | 2.03 | 3.31 | 3.46 |
| 22:45 | 3847 | Wycombe vs Fleetwood Town | 1.70 | 3.58 | 4.74 |
| 22:45 | 3866 | Solihull Moors vs Torquay | 1.95 | 3.52 | 3.46 |
| 22:45 | 3879 | Wealdstone vs Maidstone | 2.11 | 3.36 | 3.20 |
| 22:45 | 4033 | Cambridge Utd vs Morecambe | 2.02 | 3.38 | 3.48 |
| 22:45 | 4188 | Morton vs Ayr United | 2.32 | 3.18 | 2.87 |
| 22:45 | 4288 | Walsall vs Bradford City | 2.50 | 3.05 | 2.70 |
| 22:45 | 4340 | Dumbarton vs Stirling | 2.39 | 3.23 | 2.62 |
| 22:45 | 4775 | Coleraine FC vs Ballymena Utd | 1.35 | 4.43 | 7.00 |
| 22:45 | 4863 | Cheltenham vs Lincoln | 2.73 | 3.14 | 2.53 |
| 22:45 | 4908 | Stockport vs Gillingham | 1.53 | 3.75 | 5.53 |
| 22:45 | 5052 | Oldham vs Woking | 3.26 | 3.26 | 2.12 |
| 22:45 | 5230 | Yeovil vs Eastleigh | 2.88 | 3.15 | 2.38 |
| 22:45 | 5443 | Doncaster vs Harrogate | 1.95 | 3.41 | 3.41 |
| 22:45 | 5652 | Carrick Rangers vs Glentoran Belfast | 4.94 | 3.86 | 1.54 |
| 23:00 | 2862 | Reading vs Sheffield Utd | 3.75 | 3.50 | 1.86 |
| 23:00 | 3483 | Plymouth vs Derby | 2.59 | 3.35 | 2.54 |
| 23:00 | 3713 | Chelsea vs Borussia Dortmund | 1.86 | 3.50 | 3.75 |
| 23:00 | 4639 | Benfica vs Brugge | 1.40 | 4.49 | 6.59 |
| 23:00 | 5988 | West Bromwich vs Wigan | 1.56 | 3.80 | 5.40 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Machi 7, 2023

Nipashe




UKURASA 21

**Ten Hag ataka maelezo ya wachezaji kipigo Liver**

**HAWATOKI...**



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi ya mwisho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana kabla ya leo usiku kuikaribisha Vipers ya Uganda kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# FEI TOTO, YANGA SC KUKAA MEZA MOJA

●●●Sasa autambua mkataba, arudi tena TFF na mwanasheria wa Msuva akiomba kuuvunja, Morrison naye...

**Na Adam Fungamwango**

SIKU chache tu baada ya rufani yake kugonga mwamba kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi ya Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' amerejea tena katika shirikisho hilo, safari hii akiwasilisha barua ya maombi ya kutaka kuvunja mkataba na klabu yake hiyo.

Fei Toto alitinga jana kwenye ofisi za TFF akiwa na mwakilishi wake, mwanasheria Jasmin Razack, akiwasilisha barua hiyo akiomba kuvunja mkataba, ikiwa ni siku chache zimepita tangu maombi yake ya marejeo hukumu yake kuonekana hayana mashiko kisheria na kamati hiyo, hivyo kusimamia msimamo wake wa awali kama ni mchezaji halali wa Yanga.

Jasmin, ambaye amewahi kuwasimamia wachezaji mbalimbali, akiwamo Simon Msuva, alipokuwa na matatizo na klabu yake ya Wydad Casablanca ya Morocco na kumwezesha Mtanzania huyo kushinda, alikiri kuwa ni kweli mteja wake amepeleka maombi ya kutaka kuvunja mkataba na klabu yake hiyo na anaamini kuwa yatashughulikiwa kikamilifu.

"Feisal kaleta ombi lake, nina imani kwamba litashughulikiwa, nina imani kama atapata haki, nina imani na TFF kwa hiyo tusubiri, hili ombi limepokelewa hivyo tumeiachia TFF walisikilize halafu tutajua mengine. Tukumbuke kuwa chombo pekee kinachoweza kuvunja mkataba wa mchezaji ni TFF, kuna kanuni, mchezaji hawezi kuvunja mkataba wala klabu haiwezi kuvunja mkataba," alisema Jasmin.

Mwanasheria huyo hakutaka kuongea chochote kuhusu mchezaji huyo kwenda CAS, wala maamuzi yaliyopita, badala yake akasema kilichomleta yeye ni hicho tu.

"Sipo hapa kuzungumzia masuala ya CAS, napenda kuzungumzia kitu kilichopo hapa, haya maneno yamekuwa mengi, huyu kasema hili, yule kasema lile, siko tayari kuingia kwenye malumbano, ninachowaambia ni kwamba Feisal kaleta ombi la kuvunja mkataba na Yanga, ombi limepokelewa, tuwaachie TFF watatoa maamuzi, nina imani nao, kwanza sasa tusubiri maamuzi yatakayotoka.

"Maneno mengi yamesemwa kwenye hili suala, mkumbuke kuwa sisi tunajenga timu ya taifa, mpira wetu haupo sehemu ambayo sisi tunataka uwapo, tuache TFF wafanye kazi yake na wanahabari mripoti kitu kilicho sahihi," alisema mwanasheria huyo.

Awali, Yanga ndiyo iliyopeleka barua

INAENDELEA UK. 23

## Simba: Ni ushindi tu kwa Mkapa leo

**Na Saada Akida**

SIMBA imeeleza kukamilisha hesabu zake za kusaka pointi tatu leo katika mchezo wa marudiano wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers kutoka Uganda.

Wekundu hao wa Msimbazi watakuwa wenyeji katika mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, leo saa 1:00 usiku.

Simba wanahitaji pointi tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kutinga robo fainali katika Kundi D ambalo wanashika nafasi ya tatu wakiwa na pointi tatu huku Vipers FC wakiburuza mkia. Katika kundi hilo Raja Casablanca inaongoza ikiwa na pointi tisa na Horoya AC wako nafasi ya pili wakiwa na pointi nne.

Wakati Simba ikiwa kamili kwa mchezo huo, Vipers itamkosa nyota wake, Milton Karisa, ambaye alipata majeraha ya misuli kwenye mchezo uliopita ambao walipoteza kwa bao 1-0 mbele ya Simba katika Uwanja wa St. Mary's Kitende nchini Uganda.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Simba Robertinho Oliveira, alisema wamefanya maandalizi mazuri na malengo yao makubwa ni kutumia vema uwanja wa nyumbani kupata ushindi dhidi ya Vipers.

Alisema morali ya wachezaji wake ipo vizuri na wanahitaji ushindi

INAENDELEA UK. 23



9 770856 541002 >

Na Adam Fungamw